UTUNGU WA KUZAA

Na tuinamishe vichwa vyetu.

2 Mungu mpenzi, tunashukuru sana leo kwa mbubujiko mkuu wa Uwepo Wako, kati yetu, uliopo tayari. Nasi tunatarajia jambo hili, mno, na kwa wingi, alasiri ya leo. Tunashukuru kwa wimbo huu mzuri sana kutoka kwa mwanamke huyu mzuri Mkristo ambaye ameimba wimbo huu sasa hivi, na Roho Wako aliyeshuka, na tafsiri iliyotolewa. Bwana, na iwe hivyo, tunaomba. Na, Mungu, naomba ya kwamba utambariki kila mmoja wetu, pia naomba mioyo yetu ijazwe na furaha tunapoona jambo hili likitukia.

3 Mungu mpendwa, tunaomba, alasiri ya leo, ikiwa baadhi ya waliopo hapa hawako tayari kukutana na Wewe, jalia hii iwe ndiyo saa watakayofanya uamuzi huo wa mwisho na watakuja Kwako, kwa Kuzaliwa Upya. Tujalie.

4 Tubariki sisi sote, Bwana, ambao tumekuwa safarini kwa muda mrefu. Tunaomba ya kwamba utatufundisha mambo mapya kwa Neno Lako. Tupe ufahamu bora zaidi kwa Roho Wako, Bwana. Jalia Yeye aje na kulifasiri Neno. Mfasiri pekee tuliye naye ni Roho. Tunaomba ya kwamba atatujalia jambo hilo, leo. Tunaomba haya katika Jina la Yesu. Amina.

[Dada mmoja anaanza kutoa unabii. Sehemu tupu kwenye kanda-Mh.]

5 Hilo latosha. [Ndugu mmoja anazungumza na ndugu mwingine—Mh.] Ni wakati wa jinsi gani! Sijui mahali pengine bora zaidi pa kuwa, isipokuwa iwe ni Mbinguni, kwa maana tunasikia tu upako wa Huko sasa, mnaona, tukiketi pamoja katika ulimwengu wa Roho katika Kristo Yesu, tumekusanyika pamoja katika ulimwengu wa Roho.

6 Mungu na ambariki Dada Florence! Naye anapitia katika wakati wa huzuni, na mashaka; baba yake ndiyo kwanza aage dunia. Nami na—naomba, "Mungu, na ambariki mtoto huyo."

7 Pia Ndugu Demos, amebeba mizigo kwenye mabega yote mawili, na uzito wa mikutano hii yote na kadhalika. Anahitaji maombi yetu, pia. Mungu na ambariki Ndugu Shakarian!

8 Ndugu Carl Williams, kwa kweli nina furaha kuwapo hapa katika mkutano huu pamoja nawe, miongoni mwa ndugu hawa wote wazuri. Nami nilipata majaliwa ya kukutana na baadhi yao. Na sasa hii ni sehemu yangu ya kumalizia ibada, nijuavyo mimi, kwa hiyo, mbona, ninatarajia sasa kuweza kupeana mikono na baadhi ya hawa watu wazuri, na—na nipate kukutana nao, kwa maana ninatumaini kuishi Milele pamoja nao, katika N—Nchi bora zaidi.

9 Hebu—jambo kidogo tu, natumaini sitaeleweka vibaya. Wala si kwa bahati, sidhani hivyo, kwa kuwa na—nafikiri ilikuwa majaliwa, kwamba jana nilikabidhiwa zawadi na rafiki fulani hapa, kutoka kwa rafiki yangu, Danny Henry. Alikuwa ni yule mvulana . . . Siku moja, katika mkutano wa Wafanyabiashara Wakristo huko California, nilikuwa na—na mkutano. Nilikuwa nikizungumza kwa ukali sana dhidi ya ha—hali ya wakati huu.

10 Nami na—natarajia ya kwamba kila mtu anafahamu jambo hilo, sina chuki ndani ya moyo wangu. Si hivyo. La. Hakika mtafahamu simaanishi hivyo. Lakini sina budi kusema yale tu yanayonijia kusema.

11 Na halafu baada ya jambo hilo, maskini jamaa huyu, ndugu wa Kibatisti . . . Nami nafikiri yeye ni jamaa ya mchezaji fulani wa sinema. Basi alishuka kuja kunikumbatia, na kusema, "Bwana akubariki, Ndugu Branham. Ninataka kukuombea kidogo tu." Ndipo akaanza kunena Kifaransa. Wala mvulana huyo hajui hata neno moja la Kifaransa.

12 Ndipo mtu fulani akainuka, mwanamke mkubwa hivi. Kutoka . . . Nadhani alitoka Louisiana. Akasema, "Hicho ni Kifaransa."

Halafu kulikuwako na mtu kule, kasema, "Hicho ni Kifaransa."

13 Nao walikuwa wameandika ilivyokuwa. Nina nakala ya asili hapa. Na halafu, ikatokea kuwa, kijana mmoja alikuwa anakuja kutoka huko nyuma, na anasogea mbele, akitaka kuona maandishi yao. Naye alikuwa ndiye mkalimani wa U.M. wa Kifaransa. "Hicho ni Kifaransa kitupu."

14 Nami ningetaka kusoma maandishi haya. Haya ndiyo maandishi ya asili ya mmoja wao, na yalitokana na mtu huyu ambaye alikuwa amefasiri. Huenda nisiweze kutamka jina lake vizuri. Le Doux, Victor Le Doux, yeye ni Mfarasa halisi. Sasa, huo ujumbe ndio huu hapa.

> *Kwa kuwa umechagua njia iliyo nyembamba, njia iliyo ngumu zaidi, umeenda kwa hiari yako, umechagua uamuzi mzuri na sahihi, na ni Njia Yangu. Kwa sababu ya uamuzi huu muhimu sana, sehemu kubwa mno ya Mbingu inakungojea. Ni uamuzi wa fahari jinsi gani umefanya! Jambo hili, lenyewe, ndilo litakalotoa, na kutimiza, ule ushindi mkuu sana katika Upendo wa Kiungu.*

15 Nilipopata huo . . . Unajua, wakati niliposikia mara ya kwamza watu wakinena kwa lugha, ni—nisingelaumu jambo lo lote, unaona, kwa maana nimeona ni jambo la kweli. Lakini, daima nimeshangaa. Lakini wakati jambo hilo lilipotukia, na nikijua lile agizo lilikuwa ni nini, nyuma yake, ni—nilijua lilitoka kwa Mungu.

16 Halafu, ndugu yake anayeketi hapa, wakili halisi anayejulikana sa—sana, alinikabidhi zawadi kutoka kwa Danny. Danny alitoka Nchi Takatifu hivi karibuni. Naye alikuwa amelala juu ya kaburi, kaburini, hasa, mahali Yesu alikuwa amelazwa baada ya mauti Yake. Na alipofanya hivyo, alisema alianza kuwaza juu yangu. Na—na Roho wa Bwana akamjia, ndipo akakwea kwenda Mlima Kalvari ambako kule kusulibishwa kulitukia, basi akatwaa kipande cha mwamba. Ndipo akarudi na kunitengenezea jozi ya vifungo vya sijafu kutokana nacho. Nami kweli navipenda.

17 Na sasa, hili, bila shaka, Danny hajui jambo hili. Lakini, asubuhi ya leo, wakati nilipokuwa nikiomba, niliviangalia tu hivyo vifungo vya sijafu, na kila kimoja cha hivyo, kama ukiangalia, kina alama ya damu, na pia kina mstari ulionyoka moja kwa moja ndani ya kila kimoja. Na hapa kwenye ujumbe alioutoa kutoka kwa Mungu, wa njia nyofu, iliyo nyembamba. Jinsi unavyolingana, vizuri kabisa! Nilifikiri hilo lilikuwa kwa namna fulani labda la kimbinguni. Ama, kwa kweli ninamshukuru Danny. Mwambie, ndugu, jinsi ninavyofurahia jambo hilo. Na aja-. . . Jambo jingine la ajabu, nilimwomba mke wangu asubuhi niliyovaa shati, ilipaswa kuwa na vifungo vya sijafu, naye akasema, "Nilisahau kukuletea sijafu zako," kwa hiyo Bwana alinipa vingine.

18 Loo, ni maisha yenye utukufu! Sivyo, ndugu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kuenenda tu katika urahisi wa—wa Injili! Na hata hivyo, katika urahisi Wake, ndilo Jambo lililo kuu kuliko yote ninayojua. Ninajua hakuna kinacholingana Nayo. Na kwa kuwa lilifanywa rahisi, hata nikawa na nafasi ya kuingia Kwake, unaona, pia, kwa neema ya Mungu.

19 Sasa, alasiri ya leo, sitaki kuchukua wakati mwingi, kwa sababu ninajua mnaenda makanisani usiku wa leo. Nadhani, ninyi wageni wote hapa mnapaswa kuangalia kila mahali jukwaani, muwaone wahudumu hawa, nao wananinii, loo, watafurahi kuwa nanyi katika ibada zao usiku wa leo. Watawafanyia mema. Hapana shaka ulihudhuria shule fulani ya Jumapili asbuhi ya leo mjini. Na wakati tukiwa na mikutano hii, na tukiwa Wafanyabiashara wa Injili Yote, nafikiri inatubidi kuyapa makanisa yetu msaada wote tuwezao, kwa kuwa huko ndiko shughuli zetu zinakoelekea. Na, sasa, ni nyumba ya Mungu, nami natumaini mtahudhuria kanisa fulani usiku wa leo.

20 Kesho usiku ni kumalizia kwa mkutano, ninaamini, nami nadhani wametangaza mhubiri. Ambapo, nitakuwa hapa, Bwana akipenda, kusikiliza ujumbe wake.

Mungu ambariki kila mmoja wenu.

21 Sasa, mimi, sidai kuwa mhubiri. Mimi—mimi kwa namna fulani ninaninii. . . Sina elimu ya kutosha kujiita mhubiri.

Mhubiri, unaposema hivyo, wanakutarajia kuwa na digrii kadha chuoni. Na—na mimi sina kitu ila kombeo *Hili* dogo. Unaona? Mimi ninajaribu kuwafuatilia kondoo walio wagonjwa, nikiweza, kuwarudisha kwenye malisho ya Baba.

22 Kama nikifanya makosa, nisameheni. Mimi si mwanatheolojia. Simlaumu mwanatheojia. Theolo . . . Theolojia ni sawa. Ndiyo tunayohitaji. Lakini wakati mwingine ninalaumu hali ambayo tumeingia. Hilo halimwelekei mtu ye yote binafsi. Ni Ujumbe tu. La—laiti isingalikuwa ni mimi wa kuutoa. Linanihuzunisha sana, maana unajua jinsi unavyojisikia juu ya watoto wako mwenyewe. Unaona? Je! si unachukia kumkaripia mtoto, kumpigia makelele, ama cho chote kile, hata hivyo? Mimi ni mzazi, pia, nami ninajua jinsi ilivyo. Nami na—natumaini mngenisamehe.

23 Nami nawatakeni mfanye hivi. Mnapokuwa mnaketi, alasiri ya leo, nitawaomba kibali chenu. Nina maandishi mafupi, machache hapa. Kama nilivyowaambia, sina budi kufanya jambo hili, kuandika Maandiko yangu. Ilikuwa kawaida ya kwamba, ningeweza karibu kunukuu Biblia kwa moyo, lakini si sasa. Nilipitia katika vita vingi vigumu kupita kiasi, nimekuwa mzee sana kuweza kufanya jambo hilo. Lakini ninatumaini ya kwamba—ya kwamba mtanisikiliza kwa muda mfupi tu, alasiri ya leo, na kwa kweli muufungue tu moyo wenu na mjaribu kupata kile ninachochimbua. Ndipo ninafikiri litakuwa ni jambo zuri zaidi, hasa sana kwa wachungaji wa mjini na mahali mbalimbali. Na—natumaini ya kwamba mtasikiliza kwa makini sana.

24 Na sasa mfanye hivyo, fanyeni kama nifanyavyo ninapokula sambusa yangu ninayopenda sana, ya cheri. Baadhi ya nyama ninazozipenda sana, ni kuku. Lakini wakati ninapokula kipande kizuri cha sambusa ya cheri na ninakumbana na mbegu, sitaacha kula sambusa hiyo. Ninatupa tu hiyo mbegu, na kuendelea kula sambusa. Unaona? Nikifikia kwenye mfupa wa kuku; siitupi kuku. Ninatupata tu ule mfupa.

25 Kwa hiyo, vipi kama ningesema jambo ambalo huwezi kukubaliana nalo, wakati wo wote? Tupilia tu mbali sehemu hiyo. Na, ila, iangalie vizuri sana, uwe na hakika ni mfupa, sasa. Unaona? [Kusanyiko linacheka—Mh.] Na halafu hebu pia niseme, kama ni Mbegu, kumbuka, itazaa Uhai mpya. Kwa hiyo angalia kwa makini sana, na Bwana na akubariki.

26 Ndugu Carl Williams alisema jambo fulani hivi majuzi juu ya kuvunja mkutano, kuwaombea wagonjwa, jambo ambalo lingekuwa ni zuri sana. Najua jambo hilo lingekuwa zuri sana. Lakini tunaninii tu . . . hatujajiandaa hapa kwa ajili ya jambo hilo, kuleta mstari wa maombi. Na sijui kama Ndugu Oral, ama ye yote wa hao ndugu wengine wamewahi kuwa na mistari ya maombi katika mikutano ama la. Sijui. Nimejaribu jambo hilo,

mara mbili ama tatu. Lakini, kwa kawaida, kama kundi kama hili, itakubidi kusambaza kadi za maombi, unaona, ili kufanya hivyo. Maana, huwezi. Si uwanja wa michezo. Ni nyumba ya Mungu. Unaona? Imewekwa maalumu kwa ajili ya jambo hilo. Nasi . . . Wanasongamana na kusukumana. Na unachukua kadi, unawasimamisha kwenye mstari, kwa utaratibu.

27 Kwa hiyo Billy aliniuliza, kasema, "Niende nikasambaze kadi za maombi? Watu wananiomba kadi za maombi."

28 Nikasema, "La, Billy. Hebu tumwache tu Roho Mtakatifu afanye atakalo." Unaona? Hilo, unaona, na acha labda ajenge imani, na mponywe mahali papo hapo mlipo. Unaona? Lakini ninii . . . Unaona?

29 Uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo katika Injili. Wala huwezi kung'angania jambo dogo. Mtu ye yote anajua jambo hilo. Lakini wao . . . Ni chambo kinachotumiwa kuwafanya watu waamini katika Uwepo wa kimbinguni, ama Mungu, ya Kimbinguni yapo. Halafu, kwa njia hiyo, kama wanaweza kutambua Uwepo Wake, basi wanaponywa, unaona, kwa imani, kuamini jambo Hilo.

30 Sasa nataka kusoma machache kutoka kwenye Neno la Mungu, Agano Jipya. Na halafu nataka kuchukua somo kutoka kwenye Agano hili Jipya, na Andiko hili, na kuzungumza alasiri ya leo juu ya somo fulani kwa muda ki—kidogo tu. Wala sitaki kuwaweka kwa muda mrefu sana kwa ajili ya ibada usiku wa leo. Lakini kumbukeni, ninatumaini nimejifanya dhahiri. Lipeni usikizi wenu kwa muda kidogo, tafadhalini.

Sasa, kabla hatujafanya jambo hili, hebu na tuinamishe vichwa vyetu tena.

31 Mnajua, tungeweza kuimba kupita kiasi. Tungeweza kupiga makelele kupita kiasi, mpaka tupwelewe na sauti. Na tungeweza kuimba kwa wakati usiofaa, ama kupiga makelele kwa wakati usiofaa. Lakini kuna jambo moja, kamwe hatuko nje ya utaratibu wakati tunaomba. "Ninataka wanaume wasalishe kila mahali, huku wakiinua mikono iliyotakata, pasipo tashwishi." Au . . .

32 Baba, ni majaliwa makubwa sana mwanadamu aliyopata kuwa nayo, ilikuwa ni kufunga macho yake na kuufungua moyo wake, na kuzungumza Nawe. Nasi tunajua ya kwamba Wewe unasikia, kama tungaliweza tu kuamini ya kwamba Wewe unasikia. Kwa maana Yesu alisema, "Mkimwomba Baba neno lo lote katika Jina Langu, mtapewa." Hilo lilikuwa na masharti, ikiwa hatungelitilia shaka. Kwa hiyo, Baba, tusaidie kuamini, alasiri ya leo, ya kwamba ombi letu litajaliwa. Na jalia pasiwepo na shaka hata kidogo, mahali po pote. Lakini na yatimie, mambo tunayoomba. Na hiyo ni kusema, Mungu, kwa ajili ya kuliheshimu Jina Lako kuu leo, kwa kuingiza katika Ufalme Wako kila mtu aliyepotea na kila anayetangatanga aliye chini

ya sauti yetu, ama pale ambapo kanda hii itawahi kufika, huko kwenye nchi za makafiri, mahali ambako zitaenda kote ulimwenguni.

33 Ninaomba, Baba wa Mbinguni, ya kwamba hakutakuwako na mtu mnyonge miongoni mwetu leo. Wakati huduma itakapomalizika, naomba Bwana amwokoe kila mtu aliyepotea, na kuponya kila mwili mgonjwa, na kuujaza moyo wa watoto Wake kwa furaha. Hiyo ndiyo sababu tuna imani, Bwana, kuomba katika Jina la Yesu, kwa Mungu Baba yetu, kwa sababu Yeye aliahidi angesikia. Na hii ni kwa ajilia ya utukufu Wake. Amina.

34 Katika Injili ya Yohana Mtakatifu, mlango wa 17, na kuanzia kifungu cha 20, ningetaka kusoma so—somo. Nafikiri hiyo ni kweli.

> *Wala si hao tu ninaowaombea, lakini kwa wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao;*
>
> *Wote . . .*

35 Naamini nimefungua mahali pengine. Sasa, samahani kwa muda kidogo tu. Ninatafuta maombi ya Yesu ambayo . . . Ama, si maombi ya Yesu, hasa, lakini ninii Yake . . . Huenda nilikosea katika kuandika hapa kwenye maandishi yangu. Ni mahali pale ambapo Yesu aliomba ya kwamba . . . ama alikuwa akisema ya kwamba kama mwanamke katika utungu wa kuzaa kwa ajili ya kuzaliwa kwa mtoto wake, kuzaa, kuzaa mtoto.

36 Hiyo ni katika Luka ama Yohana? Jack, hiyo iko wapi? [Mtu fulani anasema, "Yohana 16."—Mh.] Yohana 16. Nadhani hiyo ilikuwa ndiyo, lakini haikusikika sana kama hiyo. Yohana 16. ["Kifungu cha 21."] Kifungu cha 21. [Mwingine anasema, "Ndiyo."] Hakika, kifungu cha 21. Hakika. Hii hapa. Yohana, Yohana Mtakatifu 16:21.

> *Wote wawe na . . .*

37 La, Ndugu Jack, hapo bado sipo. [Mtu fulani anasema, "Jaribu Yohana, kifungu cha 21." Mwingine anasema, "21." Mwingine anasema, "kifungu cha 21 cha 16." Mwingine asema, wa "16."—Mh.] Ni cha 20, 16:21. Nimefungua mlango wa 16 wa Yohana Mtakatifu, kifungu cha 21. Lakini . . . Je! nimekosea? [Ndugu fulani anasema, "Hebu nikihamishe, papo hapo kilipo."]

38 Vema, kuna vurugu katika hii, kuchanganyikana katika Biblia hii. Naam, bwana. [Ndugu fulani anasema, "Wa—wameichapisha vibaya."—Mh.] Waliichapisha vibaya. Naam, bwana. [Kusanyiko linacheka.] Unajua nini? Hiyo ni kweli kabisa. Hii hapa Biblia mpya kabisa. Ndiyo kwanza niipate. Na ina—inaninii . . . Imechapishwa vibaya. [Kurasa 1138-1139 za Biblia ya Scofield ya Ndugu Branham zilikuwa zimeshikamana. Sikiliza *Leo Maandiko Haya Yametimia* 65-0219.]

39 [Askofu mkuu wa Katoliki akiwa amesimama jukwaani, Kasisi John S. Stanley, anasonga mbele na kumpa Ndugu Branham Biblia yake, na kusema, "Tu—tulia tu. Kuna sababu kwa nini jambo hili limefanyika, nawe unajua jambo hilo. Mungu atakuonyesha jambo fulani la kuhubiri kutoka kwenye jambo hili, ambalo ni la ajabu sana."—Mh.] Vema. ["Tumia tu yangu hapa, ndugu."] Asante. Asante, asante sana. 16;21. Asante, asante sana. Hiyo ni kweli.

Mwanamke azaapo . . .

Amin, amin, nawaambia, Ninyi mtalala*, mtalia na kuomboleza, bali ulimwengu utafurahi: ninyi mtahuzunishwa, . . . huzuni yenu itageuka kuwa furaha.*

Mwanamke a—azaapo, yuna huzuni, kwa kuwa saa yake inakuja: lakini akiisha kuzaa mwana, haikumbuki tena . . . dhiki—ile dhiki, kwa sababu ya furaha ya kuzaliwa mtu ulimwenguni.

40 Asante, sana, ndugu yangu. Hakika nathamini jambo hilo. [Ndugu Branham anarudisha ile Biblia kwa yule kasisi wa Katoliki—Mh.]

41 Sasa, huko bila shaka ni kuchapishwa kimakosa hapa katika Biblia; kurasa zimewekwa vibaya. Nami niliyapata tu kwenye Biblia yangu ya zamani ya Scofield, ndipo nikaitwaa hii na kukimbilia huku juu nayo, muda mchache tu uliopita, maana mke wangu ndiyo kwanza anipe hii kama zawadi ya Krismasi.

42 Sasa, nataka ku—kuzungumza alasiri ya leo juu ya somo fulani ambalo nilitangaza: *Utungu wa Kuzaa*. Sasa, hilo linasikika baya sana, lakini limo katika Biblia.

43 Ninaamini ya kwamba Yesu hapa alikuwa akinena juu ya, kama alivyosema, "Mtahuzunishwa, lakini huzuni yenu itageuka kuwa furaha," akizungumza na wanafunzi Wake hapa, akijua ya kwamba kuzaliwa kwa—kwa Ukristo kulikuwa kunakuja. Na sasa ya kale hayana budi kufa, kusudi yaliyo mapya yazaliwe. Ukiwa na kitu cho chote kinachozaa, hakina budi kusikia uchungu na dhiki. Na bila shaka walikuwa watapitia katika uchungu wa dhiki na maumivu makuu, kutoka kwenye torati kuingia katika neema.

44 Kawaida, uzazi wa kawaida ni mfano wa uzazi wa kiroho. Mambo yote ya kawaida ni mfano wa yale ya kiroho. Nasi tunaona, kama tukiangalia hapa nje kwenye—kwenye ardhi, na kuona mti katika nchi, ukikua, ukishindania uzima. Hilo linaonyesha ya kwamba kuna mti, mahali fulani, usiokufa, kwa sababu una—unalilia jambo hilo.

45 Tunaona watu, haidhuru wao ni wakongwe namna gani, ni wagonjwa jinsi gani, wana hali gani, wanalia, wapate kuishi, kwa kuwa inaonyesha kuna uhai mahali fulani ambapo tunaishi—tunaishi milele. Angalia jinsi lilivyo kamilifu.

46 Sasa, katika Yohana wa Kwanza 5:7, ninaamini ndipo, kama sijakosea, ilisema, "Wako watatu washuhudiao Mbinguni: Baba, Neno, na Roho Mtakatifu; watatu hawa ni Mmoja. Wako watatu washuhudiao duniani, hao ni maji, Damu, na Roho, hawa hupatana kwa habari moja." Sasa angalia. Hao watatu wa kwanza *ni* Mmoja. Hao watatu wa pili ni wa duniani, ambao *hupatana* kwa habari moja. Huwezi kuwa na Baba bila Mwana; huwezi kuwa na Mwana bila kuwa na Roho Mtakatifu. Lakini unaweza kuwa na maji bila Damu, na Damu bila Roho.

47 Nafikiri, kote katika nyakati zetu, hii imethibitika kwamba ni kweli; maji, Damu, Roho; kuhesabiwa haki, utakaso, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo hufananishwa au inafanya ninii . . . au, na kivuli, ambayo hondoa kutoka kwenye kuzaliwa kwa maumbile.

48 Angalia wakati mwa—mwanamke ama cho chote katika utungu, kwa ajili ya kuzaa. Jambo la kwanza linalotukia, ni kutoka kwa maji, kuzaliwa kwa kawaida; jambo la pili ni damu; halafu uhai unatokea. Maji, damu, roho; na hiyo hufanya kuzaliwa kwa kawaida, kwa maumbile.

49 Na ndivyo ilivyo katika ulimwengu wa roho. Ni maji; kuhesabiwa haki kwa imani, kumwamini Mungu, kumpokea Yeye kama Mkombozi wako binafsi, na kubatizwa. Pili, ni kutakaswa kwa roho, ambapo Mungu huisafisha roho na vitu vyote vya ulimwengu, na tamaa ya ulimwengu. Na ndipo Roho Mtakatifu anaingia na kutoa Uzao mpya na kukijaza chombo hicho kilichotakaswa.

50 Kwa mfano, ni namna hii. Sasa, jambo hilo, niliwaambia. Kile usichoamini, weka kando, halafu ule sambusa. Angalia. Sasa, gi—gilasi iko kwenye ua wa kuku. Huichukui tu hiyo na kuiweka mezani mwako na kuijaza na maji ama maziwa. La. Unapoichukua, ni kuihesabia haki. Ukiiosha, ni kuitakasa, maana neno la Kiyunani *kutakasa* ni neno lenye sehemu mbili, ambalo linamaanisha "kuoshwa, na kutengwa kwa ajili ya kutumika." Si *katika* huduma; *kwa ajili ya* huduma. Ndipo wakati unapoijaza, inatumika.

51 Samahani kwa jambo hili sasa, si kwa ajili ya kuudhi. Hapo ndipo ninyi Wapilgim Holiness, Wanazarayo mlishindwa kupiga hatua mpaka kuingia kwenye Pentekoste. Mlisafishwa kwa kutakaswa; lakini mlipokuwa tayari kuwekwa katika huduma, kwa karama za kunena katika lugha na vitu vingine, mlizikataa hizo, mkarudi zizini tena. Mnaona? Sasa, hivyo—hivyo ndivyo inavyotukia. Daima inafanyika hivyo.

52 Sasa, si kuwalaumu ninyi sasa, lakini ninii—ninataka kutoa jambo hili moyoni mwangu. Na hilo limekuwa likinichoma tangu nilipokuwa hapa, kwa hiyo ni heri nilitoe. Ninii tu, kama neema ya Carl, na Demos na hao wengine, na yenu nyote, ni—nitajaribu

kukomboa nafsi yangu kutokana na jambo hilo, unaona, ndipo basi ni juu yenu.

Ya kawaida, yakiwa mfano wa ya kiroho.

53 Sasa, tunaona basi, na amezaliwa kabisa. Wakati mtoto mchanga, kwa kawaida . . . Sasa wakati maji yanapovuja, haikubidi kumsaidia sana. Na wakati damu inapotoka, haikubidi kumshughulikia sana. Lakini, ili uhai uingie ndani ya mtoto huyo mchanga, huna budi kumpiga kofi la matakoni, na kumfanya apige makelele. Na hiyo ni . . . Sasa, bila elimu, kama vile ndugu zangu hapa wamefunzwa vizuri sana, yao, lakini mimi sina budi kuchukua mambo ya asili kutoa mfano wake. Na haya basi. Hivyo ndivyo ilivyotendeka. Inatakiwa kupigwa kofi halisi, kuingiza hili ndani yao.

54 Sasa, chukua ninii dogo, kitu fulani cha kushtua. Labda, haitakulazimu kumpiga kofi, lakini mshtue tu kidogo. Wazo lenyewe la Yeye kuzaliwa, wakati mwingine, litafanya jambo hilo. Mnyakue, mtikise. Asipoanza kupumua, mpige kofi kidogo, ndipo atapiga mayowe, katika lugha isiyojulikana, kwa nafsi yake, nadhani. Lakini, yeye—yeye, hata hivyo, naye anapiga makelele.

55 Nami nafikiri kama mtoto akizaliwa tu akiwa—akiwa kimya, hana sauti, hana mwamsho, huyo ni mtoto mfu.

56 Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, ule mfumo; tuna watoto wengi kupita kiasi waliozaliwa wamekufa. Hiyo ni kweli. Wanahitaji kofi la Injili, unaona, na hiyo basi ili kuwaamsha, kuwafanya wajirudie, kusudi Mungu aweze kuwapulizia ndani yao pumzi ya Uhai. Na sasa tunaona ya kwamba hilo ni kweli kabisa. Ni theolojia mbichi, bali ni Kweli, hata hivyo.

57 Kwa hiyo, angalia, katika kuzaliwa kwa mbegu, ile mbegu ya kale haina budi kufa kabla ile mpya kuweza kuzaliwa. Kwa hiyo, basi, kifo ni jambo gumu, wakati wo wote. Kwa hiyo, ni kichungu. Kinahuzunisha. Kuzaliwa ni jambo lile lile, kwa maana unaleta uhai ulimwenguni, na ni—ni kuchungu.

58 Yesu alisema ya kwamba Neno Lake lilikuwa ni mbegu ambayo mpanzi alitoka akaenda kupanda. Sasa, sisi sote tunajua jambo hilo. Nami ninataka kufundisha jambo hili kama somo la shule ya Jumapili, maana ni Jumapili. Angalia, basi, Neno hili, likiwa ni mbegu. Lakini, kumbukeni, mbe—mbegu huleta tu uhai mpya hapo inapokufa.

59 Na hiyo ndiyo sababu ilikuwa ni vigumu sana kwa hao Mafarisayo kumfahamu Bwana wetu Yesu Kristo, kwa kuwa walikuwa chini ya torati. Na torati ilikuwa ni Neno la Mungu katika umbo la mbegu. Lakini wakati Neno lilipofanyika mwili, na likawa, si torati, lakini neema. Sasa, neema na torati haviwezi kudumu wakati ule ule. Maana, neema iko juu mbali sana na torati, torati hata haimo kwenye picha. Na kwa hiyo ni vigumu sana kwa hao Mafarisayo kufia torati yao, kusudi neema

ipate kuzaliwa. Lakini haina budi kuondoka. Sheria hizo mbili haziwezi kuwapo pamoja.

60 Hakuwezi kuweko na sheria inayosema ya kwamba unaweza kutumia selo hii, na nyingine inayosema unaweza kuitumia; moja inasema unaweza, nyingine inasema huwezi. Hizo, haina budi iwe ni sheria moja kwa wakati mmoja. Labda wakati mmoja ungaliweza kuipitia; kwa uangalifu, upite katika hiyo. Lakini wakati huu ni nyekundu. Simama! Unaona? Na kwa hiyo hakuwezi kuweko na sheria mbili zinazofanya kazi wakati ule ule.

61 Sasa, tunaona ya kwamba daima...Mawazo yangu sasa kwenu, inachukua uchungu, dhiki, adha. Waangalie hao Mafarisayo waliokufia hiyo torati, kupitia kwenye uchungu, dhiki, adha.Lakini ni lazima iwe hivyo.

62 Sasa, tunaona ya kwamba mvua inayoleta matunda juu ya nchi, "Inazaliwa," kama mshairi alivyosema, "katika mashamba ya radi, katika anga zilizochafuka, zenye mawingu mazito hapa na pale." Lakini kama hatungalikuwa na ngurumo na anga zilizochafuka, lile tone dogo la mvua lililotoneshwa ambalo limeinuliwa kutoka baharini na kutoneshwa kutoka kwenye chumvi, halingezaliwa. Inahitaji hiyo radi, milipuko ya ngurumo; kitu hicho cha kutisha kilichochafuka, kinachoparuza, kuzaa lile tone la petali nyororo la maji. Kuzaliwa kunahitaji uchungu. Kunahitaji kufa. Na wakati mawingu yanapokufa, mvua inazaliwa, kwa kuwa mvua ni sehemu ya wingu hilo. Moja halina budi kutoweka kusudi lingine lipate kuishi.

63 Sasa, na ndugu zangu hapa, baadhi yao waliweza, wangeweza kukupa kanuni zote za vitu hivyo. Mimi siwezi.

64 Sasa hebu na tuingilie jambo lingine, kwa thibitisho dogo tu. Ninafikiri moja ya maua yaliyo mazuri sana...Kila mtu ana mawazo yake kuhusu hayo. Lakini nafikiri ua lililo zuri sana ambalo nimepata kuona, ni kule nyuma mashariki, yungiyungi letu la kidimbwini. Ni wangapi waliopata kuona yungiyungi la kidimbwini? Loo, hakuna kitu kama hilo, kwangu mimi. Lakini ulipata kuona hilo yungiyungi la kidimbwini lilivyopaswa kuwa. Ninawazia juu ya yale Yesu aliyosema, "Fikirini yungiyungi, jinsi linavyofanya kazi na kusokota, lakini hata hivyo nawaambia, ya kwamba, Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo ya haya." Kwa kuwa, utukufu wa Sulemani na mavazi yake yote yalikuwa ya kujitengenezea. Lakini yungiyungi, katika uzuri wake, linafanywa zuri na uhai, si vitu fulani vya kujipaka vya kujitengenezea, kujipaka rangi.

65 Ni kama vile tu wanawake wetu, sidhani inawabidi kuwa na rangi hizi zote za kijani za kujipaka, mwajua, vikonyeza macho, mwajua, nje namna hiyo, na rangi hizo zote za makucha

ama—ama sivyo, ninachanganyikiwa na vitu hivyo, vyote usoni mwako, kukufanya mrembo. Urembo ni vile urembo ufanyavyo. Kama utaongeza Matendo 2:4 kidogo, uchanganye pamoja, Yohana 3:16 kidogo, vitashinda cho chote ambacho Max Factor iliwahi kujaribu kutengeneza. Unaona? Mumeo atakupenda zaidi; watu wengine wote watakupenda; nina hakika Mungu atakupenda.

66 "Yungiyungi," Yeye alisema, "fikirini, jinsi limeavyo, linavyofanya kazi, halina budi kujisukuma juu." Maskini yungiyungi hili dogo la kidimbwini, angalia mahali linapopitia; uchafu, vinyaa, matope, maji ya matope, maji machafu. Linajipenyeza kupitia hayo yote, chembechembe hii ya uhai, likijipenyeza kutoka kilindi cha kidimbwi ambamo mna vyura na—na ghasia nyingi, na halafu linajipandisha kupitia katika hayo yote. Lakini wakati linapofikia kwenye uwepo wa jua, linazaliwa. Maskini mbegu hiyo ndogo inafunguka ikawa hai. Haiwezi kufanya hivyo mpaka ipitie katika hatua hizo zote. Haina budi kupitia kwenye jambo hilo. Hilo ndilo linalolitengeneza, ni kwa sababu jua lenyewe ndilo linalolivuta juu. Na hapo linapofikia juu ya maji machafu kabisa, na vinyaa, na kadhalika, ndipo linafurahi sana. Linatoa tu uhai wake bure. Na ni uhai unaopendeza wakati linapofikia kwenye uwepo wa hilo linalolivuta juu.

67 Nafikiri huo ni mfano mzuri wa maisha ya Kikristo. Wakati, Kitu fulani kinakuvuta kutoka katika ulimwengu, mpaka siku moja unazaliwa moja kwa moja katika uwepo Wake, kwa Roho Mtakatifu. Ni jambo zuri jinsi gani! Ukijaribu kulisaidia, unaliua.

68 Kama vile kifaranga kidogo cha kuku kinapozaliwa, unajua, kama uliwahi kuona mmoja wa jamaa hao wadogo, nchani kabisa mwa mdomo wake mdogo, ama ndege ye yote anayezaliwa kutoka kwenye yai. Li—linaninii. . . Linakua, hili ganda la kale la yai. Zile sehemu za ndani za mayai zilizokomaa sana ha—hazina budi kuoza. Naye hana budi kuchukua maskini mdomo huu mdogo, na kuparuza-paruza mpaka anavunja lile ganda. Tunakuita huko, kujikokota nje, kule chini Kentucky ninakotoka. Kujikokota atoke nje. Kamwe hawajapata njia nzuri zaidi. Unaona? Unaona? Kwa nini? Ni njia iliyoandaliwa na Mungu. Ukijaribu kumsaidia, utamwua. Ukilivunja ganda atoke, atakufa. Unaona? Hana budi kufanya kazi, kujitahidi, na kuvunja atoke.

69 Hivyo ndivyo Mkristo anavyopaswa kufanya. Si swala la mtu eti kukupa mkono, kukuingiza. Inakubidi ukae pale mpaka ufe, uoze, na uzaliwe katika Ufalme wa Mungu. Ndio njia aliyoiandaa Mungu. Huingii kwa kitabu, ama kupeana mikono, na kujiunga, kuhojiwahojiwa, kujilazimisha. Ina—inakubidi tu kuondoka kwenye ganda hilo la zamani. Angalia, hawajapata njia nzuri zaidi.

70 Hawakupata njia bora zaidi ya mtoto mchanga kupata kile anachotaka mbali na njia ya Mungu kwa jambo hilo. Sasa, wakati mtoto huyo mdogo anapozaliwa, ungeweza kuweka kengele chini hapa karibu na kitanda chake kidogo, useme, "Mwanangu mdogo, katika njia hii mimi ni mwa—mwanatheolojia. Nimesoma vitabu juu ya kulea mtoto mchanga. Na, hebu nikwambie, wewe ni mtoto wa kisasa. Umezaliwa katika nyumba ya kisasa, na mzazi wa kisasa. Unaposhikwa na njaa, ama unamhitaji mama ama mimi, piga tu kijikengele hiki." Haitafua dafu hata kidogo. Jinsi tu yeye anavyoweza kupata anachotaka, ni kukililia. Hiyo ndiyo njia ya Mungu.

71 Na hivyo ndivyo tunavyopata tunachotaka, ni kukililia. Lia. Usione haya. Sema, "Nina njaa ya Mungu." Usijali kama mashemasi, wachungaji, ama wo wote walio karibu, piga makelele, hata hivyo. Akina Jones wameketi pale; inaleta tofauti gani? Lia kabisa, hiyo ndiyo njia tu iliyopo ya kukipata, mpaka upate msaada. Yeye alifundisha jambo hilo wakati alipokuwa hapa duniani, mwajua, kuhusu yule hakimu dhalimu.

72 Tone dogo la umande, sijui fomyula yake. Labda kungekuwako na mwanasayansi hapa wa . . . Nitasema tu jinsi ninavyofikiria. Huenda ikawa ni namna fulani ya anga lililochafuka kwa mawingu yaliyosongamana katika usiku wenye giza, nayo yanaanguka chini. Na yakianguka, tone linazaliwa usiku. Lakini asubuhi, liko pale, baridi, na linatatetemeka, kwenye unyasi mmoja mdogo, ama likining'inia kwenye kamba yako ya kuanikia nguo. Lakini hebu jua na liwake mara moja, je! uliona jinsi linavyoshikwa na furaha? Linametameta na kutetemeka. Kwa nini? Linajua ya kwamba hilo jua ndilo litakalolivuta na kulirudisha mahali lilipokuwa hapo mwanzo.

73 Vivyo hivyo na kila mwanamume ama mwanamke aliyezaliwa na Roho wa Mungu. Kuna jambo fulani juu yake, wakati Nuru inaposambaa juu yetu, kwamba tunashikwa na furaha, kwa maana tunajua tunarudi mahali tulipotoka, kutoka kwenye kifua cha Mungu.

74 Linaweza kumetameta kwa furaha, wakati jua linapoliwakia, bila shaka, likijua linaelekea lilikotoka.

75 Mambo madogo ya kijinga, lakini tungaliweza kuendelea nayo, lakini hebu tuone jambo lingine.

76 Tunajua ile mbegu ya zamani inaninii, haina budi, kabla ile mbegu mpya haijaweza kutoka kwenye ile mbegu ya kale, haina budi kuoza, kabisa. Si kufa, tu, bali kuoza baada ya kufa. Tunajua jambo hilo kuwa ni kweli.

77 Ni jambo lile lile katika Kuzaliwa upya. Kamwe haturudi nyuma, lakini tunasonga mbele unapozaliwa mara ya pili. Na hiyo ndiyo sababu ninafikiri, leo, tunaninii (wengi sana) si wengi sana, hasa, Wanazaliwa upya halisi, ni kwa sababu

ile mbegu, labda, italihurumia Neno ama mtu, lakini wao hawataki kuoza kutoka kwenye ule utaratibu wa zamani ambamo waliokuwamo. Hawataki kutoka mle. Wao wanataka kuishi katika utaratibu wa zamani, na kudai Kuzaliwa upya, ama Ujumbe wa wakati huo. Tuliona jambo hilo chini ya wakati wa Luther, Wesley, Wapentekoste, na nyakati nyingine zote. Wao wangali wanajaribu kushikilia kwenye ule utaratibu wa kale, na kudai jambo Hili. Lakini utaratibu wa wakati wa kale hauna budi kufa, kuoza, kusudi upate kuleta ule mpya. Wao wangali wanataka kushikilia.

78 Angalia. Wanajua utaratibu wa kale umekufa, lakini wao hawataki kamwe kuoza watoke kwake. Sasa, kuoza, ni wakati unapoondolewa kabisa. Wakati ninii. . .*Dai* linapofanywa, ya kwamba wao wamezaliwa upya, lakini dai ni ishara tu iliyotunga mimba. *Kuoza*, kunaleta Kuzaliwa upya. Hatuna budi kuoza tutoke kwake, kama tu vile tulivyofanya katika nyakati zote, kupitia wakati wa Wesley, na wengine wote.

79 Lakini jambo ni kwamba, baada ya huko Kuzaliwa upya kuzaliwa, Wesley ama. . .Luther alitokea na neno moja, "Wenye haki wataishi kwa imani." Vema, yeye hangeweza tena kushikilia kwenye ule utaratibu wa kale. Ilimbidi atoke kwake.

80 Na wakati Wakalvini walipolifikisha kanisa la Kianglikana katika hali kama hiyo, chini ya fundisho la Kalvini, mpaka Mungu alipoinua fundisho la Waameni, ambalo lilikuwa ni John Wesley. Ule utaratibu wa kale ulilazimika kufa, kusudi ule mpya upate kuja.

81 Na wakati wa Wesley ulipoisha, na nyakati zote ndogo, ama majani yaliyochipuka kwenye ubua, ama kishada, katika wakati wa Wesley. Unaona, wakati Pentekoste ilipotoka pamoja na kurudishwa kwa karama, iliwabidi watoke kwenye Baptisti, Presbiteri, Pilgrim Holiness, Wanazarayo, kanisa la Kristo, linavyojiita, na hayo yote. Iliwabidi watoke katika hayo, waoze kabisa, kusudi wakubali Kuzaliwa upya.

82 Sikuzote wewe unaitwa mwenda wazimu. Lakini ni kama alivyosema Paulo wakati alipooza akatoka kutoka kwa kile alichodai kwanza. Kasema, "Kwa njia ile ambayo waiita uzushi, ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa baba zetu." Katika njia ile ambayo waiita uzushi! Unaona? Yeye alikuwa amekubali Uzima mpya, kwamba Agano la Kale lilikuwa limezaa lile Jipya, naye ilimbidi kuoza atoke kwenye lile la Kale na kulifanya tu kivuli. Kusudi awa. . .

83 Huko ndiko tu mahali tuliko sasa. Sasa, nivumilieni. Lakini hilo ndilo wazo langu. Makanisa yamekuwa ya kimifumo sana hata huwezi kuingia kwenye moja isipokuwa wewe ni mshiriki wake. Huna budi kuwa na kadi ya ushirika, ama namna fulani ya kitambulisho. Na kwa kuamini jambo hili, mlango tu ambao karibu umefunguliwa kwa ajili yangu ni huu wa

Wafanyabiashara. Na mradi tu wao si madhehebu, ninaweza kwenda pamoja nao, lakini, na kuuleta Ujumbe, ninaojisikia uko moyoni mwangu, kwa watu. Lakini yamekuwa ya kiutaratibu sana. Nami nawapenda ninyi Wapentekoste. Na Pentekoste si madhehebu, kwa vyo vyote. Mnajiita tu wenyewe hivyo. Pentekoste ni ujuzi wala si madhehebu.

84 Lakini, mnaona, jambo ni kwamba, ni vigumu sana kwa watu wengi. Wakati wanapoliangalia na kuliamini, na kuliona limeonyeshwa dhahiri sana na Mungu, katika Neno, hata hivyo, ni vigumu sana kuoza kabisa na kutoka katika kitu hicho ulichokuwa ndani yake. "Nifanye nini? Nitapata wapi riziki yangu?"

85 Ati nini? Mungu ndiye riziki yako. Mungu ndiye kitu cha kushikilia. "Utafuteni kwanza Ufalme wa Mungu, na haki Yake." Nitaliachia hapo. Mnajua ninalozungumzia.

86 Tunaambiwa na manabii wa Mungu ya kwamba tutakuwa na nchi mpya, Mbingu mpya na nchi mpya. Kama ukitaka Maandiko kwa hayo, ni Ufunuo 21. Ningeweza kuwanukulia, ninalo hapa. Yohana alisema, "Niliona Mbingu mpya na nchi mpya: kwa kuwa mbingu ya kwanza na nchi ya kwanza zilikuwa zimepita." Ilikuwa imeondoka. Sasa, kama tutakuwa na nchi mpya, nchi ya zamani na nchi mpya haviwezi kudumu kwa wakati ule ule. Ama, ulimwengu mpya na ulimwengu wa kale haviwezi kudumu wakati mmoja. Hakuwezi kuwako na taratibu mbili za ulimwengu wakati ule ule. Sasa, kusudi upate nchi mpya, ile ya zamani haina budi kufa. Sasa, kama ile ya kale haina budi kufa, basi inapata utungu wa kuzaa kwa ajili ya ile mpya sasa.

87 Halafu kama daktari alienda kumpima mgonjwa aliyekuwa na utungu wa kuzaa sasa, ile...moja ya mambo ambayo daktari angefanya. Ambapo, ninazungumza mbele ya wawili ama watatu, niwajuao, madaktari wazuri wa madawa hapa, madaktari Wakristo. Nami ni—ni—ningewaulizeni jambo hili. Moja ya mambo ambayo daktari hufanya, baada ya kuwa amempima mgonjwa, ni kupima muda wa utungu, utungu wa kuzaa. Yeye hupima muda wa utungu, jinsi mmoja unavyokaribia mwingine, jinsi kila mmoja unavyokuwa mchungu zaidi. Mmoja ni mkali zaidi kuvumilia kuliko huo mwingine. Unaofuata, mkali zaidi, unakaribia karibu zaidi na mwingine. Hivyo ndivyo anavyopima hali hiyo, kwa utungu wa kuzaa.

88 Vema, kama ulimwengu hauna budi kuondoka kusudi ulimwengu mpya upate kuzaliwa, hebu na tuchunguze baadhi ya utungu wa kuzaa tulio nao duniani, na ndipo tutaona tuko katika siku gani nayo imeenda umbali gani katika utungu wake.

89 Vita vya Kwanza vya Dunia vilionyesha utungu mkali sana wa kuzaa. Vilionyesha mmoja wa utungu wa kwanza wa kuzaa wa kuingia kwake katika uchungu wa uzazi. Kwa sababu

wakati huo kwake, tulikuwa tumeleta mabomu, na tulikuwa na bombomu, na gesi ya sumu. Nanyi mnakumbuka. Labda wengi wenu hawawezi. Nilikuwa mvulana mdogo tu mwenye umri wa miaka kama minane hivi, lakini ninakumbuka wao wakizungumza juu ya hizi gesi za haradali na klorini, na kadhalika. "Jinsi ilivyoonekana kana kwamba ingeanza na," wao wakasema, "ingeiteketeza dunia nzima. Ingeua kila mtu. Vema, huenda ikawa ni ku—ku—kuachiliwa kwa hiyo, upepo tu ukiivumisha kote duniani." Na jinsi kila mtu alivyoogopa mno silaha hiyo kuu ya gesi ya sumu! Dunia ilipitia hayo, na ikawa na utungu wake wa kwanza wa kuzaa.

90 Nasi tunaona sasa, tumekuwa na vita vya pili, Vita vya Dunia, na uchungu wake ulikuwa mkuu zaidi. Unakuwa wa kutisha zaidi wakati wote, utungu wa kuzaa wa dunia. Dunia ilikuwa karibu iangamie, wakati wa bomu la atomiki, kwa maana lingeangamiza mji mzima. Utungu ulikuwa ni mkubwa zaidi kuliko uchungu wa Vita vya Kwanza vya Dunia, katika kuiharibu nchi.

91 Sasa, inajua ya kwamba wakati wake wa ukombozi umekaribia. Hiyo ndiyo sababu ina wasiwasi sana, imefadhaika, jinsi ilivyo, ni kwa sababu kuna bomu la haidrojeni, na makombora hewani yanayoweza kuuangamiza ulimwengu mzima. Taifa moja linaliogopa jingine, haidhuru ni dogo vipi. Wana hayo makombora wanayodai yataninii tu . . . Moja ya hayo. Wanaweza kuyaongoza kwa nyota na kuyaangusha mahali po pote ulimwenguni wanapotaka.

92 Urusi, kama nilivyosikia kwenye taarifa ya habari, hivi majuzi, inadai ya kwamba inaweza kuliangamiza taifa hili, na—na kuzuia hizo atomi ama vitu hivyo kuangamiza taifa lake. Hatujui la kufanya juu ya jambo hilo. Kila mtu anatoa madai haya, na ndivyo ilivyo.

93 Sayansi ya watu imeingia katika maabra makuu ya Mungu, hata watajiangamiza wenyewe. Mungu anaruhusu, daima huruhusu hekima ijiangamize yenyewe. Mungu haangamizi cho chote. Mwanadamu hujiangamiza kwa hekima, kama alivyofanya hapo mwanzo, akichukua hekima ya Shetani badala ya Neno la Mungu.

Sasa, dunia inajua haina budi kuangamia. Haiwezi kustahimili jambo hilo.

94 Urusi, naamini, ingeliangamiza taifa hili leo, kama ilifikiri ya kwamba ingeweza kuliangamiza, halafu ijihifadhi yenyewe. Yo yote ya mataifa hayo madogo yangeweza kufanya jambo hilo. Lakini, wanaogopa, kwa sababu wanajua ya kwamba ulimwengu huu hauwezi kusimama katika mzunguko wake chini ya hali kama hizo.

95 Kwa hiyo, ulimwengu unajua ya kwamba utungu wake wa kuzaa ni mkubwa sana, hauna budi kuangamia. Kutakuwa na

kuzaliwa kupya, kuzaliwa, karibuni. Ninashukuru kwa ajili ya jambo hilo. Nimechoshwa na huu. Mtu ye—yeyote anajua ya kwamba—ya kwamba hapa ni mahali pa mauti na huzuni, na kila namna ya hitilafu, na kadhalika. Ninafurahi ya kwamba hauna budi kuangamia. Ninafuraha ya kwamba wakati huo umekaribia. Kama Yohana, wa kale, alivyosema, "Hata hivyo, na uje, Bwana Yesu."

96 Sasa, haina budi kuoza, bila shaka, kama nilivyosema, kusudi ilete uzao mpya. Angalia vile ilivyooza. Angalieni, ndugu zangu! Imeoza kabisa. Siasa zake na taratibu zake zimeoza ziwezavyo kuwa. Hakuna mfupa mzima ndani yake, katika taratibu zake za ulimwengu, siasa zake na siasa zake za kidini, na cho chote kile. Mmoja anasema, "Mimi ni wa Democrat. Mimi ni wa Republican. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti." Mbona, kitu hicho chote kimeoza kabisa. Hakina budi kiangamie. Haiwezi kusimama. Kama ukimweka George Washington fulani ama Abraham Lincoln katika kila nchi katika Marekani hii, haingeweza kurudi bado. Haikomboleki.

97 Kuna jambo moja tu linaloweza kuisaidia, hilo ni kule Kuja kwa Muumba. Amina.

98 Inajua haina budi kuangamia. Iko katika uchungu na dhiki. Mtu hajui la kufanya. Mmoja anaangalia *huku*, na mwingine *kule*, na kila kitu. Mmoja anamwogopa mwingine. Mmoja akijaribu kufanya jambo fulani litakalomwangamiza *huyu*. *Huyu* akijaribu kunena kinyume cha *yule*, kumwangamiza huyo mwingine. Mpaka, sasa wameiweka mikononi mwa watu wenye dhambi, ambao wangeweza kuiangamiza dunia nzima katika muda wa dakika tano. Unaona? Kwa hiyo inajua haiwezi kustahimili jambo hilo. Watu wanajua haiwezi kulistahimili. Na ulimwengu unajua ya kwamba watafanya hivyo.

99 Litatukia, kwa kuwa Mungu alisema litatukia. "Mbingu zote na nchi zitateketezwa kwa moto." Itakuwa ni kufanywa upya kwa kitu hicho chote, kusudi ulimwengu mpya uzaliwe. Mungu ametabiri jambo hilo.

100 Imeoza, katika taratibu zake zote, na haina budi kufanya hivyo, kuoza kabisa.

101 Hiyo ndiyo sababu yake, nilisema, ina wasiwasi sana na imeiva usoni, na inafadhaika. Na matetemeko ya ardhi, kila mahali, huku na huko katika pwani. Na mawimbi makubwa huko Alaska, na kutetemeka huku na huko katika pwani, kwa matetemeko ya ardhi na kadhalika. Na watu wakiandika, "Je! tuhame? Je! tuhame?" Unaona? Hawajui la kufanya. Hakuna mahali pa salama ila Pamoja, hapo ni katika Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai. Na kuna jambo moja tu ambalo ni mahali pa salama, na hilo ni Yeye. Wote walio nje ya Hapo wataangamia, kwa hakika tu kama Mungu alivyosema.

102 Sasa hebu na tuangalie kwenye Kitabu cha Daktari, kama iko katika hali ya namna hii, na tuone kama jambo hili linapaswa kutukia wakati nchi mpya itakapozaliwa. Mathayo 24, katika Kitabu cha Daktari, ambacho ni Biblia, na hebu tuone yale yaliyotabiriwa, kwamba dalili zake zingekuwa ni zipi.

103 Sasa, kama daktari anajua dalili za kuzaliwa kwa mtoto . . . Na kukaribia tu wakati ambapo mtoto anapaswa kuja, anatayarisha kila kitu, kwa maana anajua ya kwamba huo ni wa—wakati wa mtoto kuzaliwa. Kwa sababu, dalili zote zinaonyesha; ma—maji yametoka, damu. Na sasa ninii . . . Ni wakati umewadia. Mtoto ameshuka, na ni wakati wa mtoto kuzaliwa umewadia. Na kwa hiyo yeye huweka kila kitu tayari kwa ajili yake.

104 Sasa, Yesu alitwambia vile hasa ingetukia kwenye wakati huu. Alitwambia, katika Mathayo 24, ya kwamba Kanisa, Kanisa la kweli, na kanisa hilo lingine, lingekuwa . . . na Kanisa la kawaida, Kanisa la kiroho, "Wangefanana sana, hao waigaji, mpaka ingewapoteza walio Wateule, kama yamkini." Jinsi ambavyo ilikuwa katika siku za Nuhu, "Jinsi walivyokuwa wakila, wakinywa, wakioa, na kuolewa," na utovu huu wote wa uadilifu wa ulimwengu tunaouona siku hizi. Biblia, kile Kitabu, Kitabu cha Daktari kilisema ingetukia. Kwa hiyo, tunapoona haya yakitukia, tunajua ya kwamba kuzaliwa kumekaribia. Hakuna budi kutukie. Naam, bwana. Sasa, tunaangalia jambo hilo, kama—kama taifa; si kama taifa, bali ulimwengu.

105 Sasa, Israeli, kanisa, hebu na tuanze nayo kwa dakika chache. Na hebu tuifuate kwa dakika kumi zijazo, labda. Israeli ilipata utungu wa kuzaa chini ya kila nabii aliyekuja duniani. Ilipata utungu wa kuzaa kwa Ujumbe wake. Ilifanya hivyo kwa nini? Nabii alikuwa na Neno. Nayo—nayo ilikuwa imepanda upuuzi mwingi sana na kuunda mashirika mengi sana ya kwake, mpaka nabii huyu akaitikisa hata kwenye msingi wake. Walichukiwa na kila mtu. Kwa hiyo, basi, wakati Mungu alipomtuma nabii, kanisa lenyewe liliingia katika utungu wa kuzaa. Kwa maana, nabii, "Neno la Mungu linamjia nabii, na yeye peke yake." Hiyo ni kusema, Neno lililonenwa kwa ajili ya siku hiyo hudhihirishwa na nabii wa wakati huo, imekuwa hivyo daima. Na, makanisa, wanajenga mashirika mengi sana kwenye Neno, hata akaitikisa ikatoka kwenye msingi wake wakati alipokuja. Ilipata utungu wa kuzaa.

106 Ilikuwa kitu gani? "Rudini kwenye Neno! Rudini kwenye Uhai! Madhehebu hayana Uzima. Neno la Mungu pekee ndilo lililo na Uzima. Taratibu zilizojengwa kulizunguka, ambapo hapana Uzima. Neno ndilo linalotoa Uzima. Ujumbe wake uliwatikisa Wateule wakarudi kwenye Neno. Kundi dogo litatoka na kuamini. Wakati fulani, labda . . . Katika wakati wa Nuhu, ni kama watu wanane hivi. Lakini, hata hivyo, Mungu

aliwatikisa waliosalia. Na, kuangamiza, hao wengine iliwabidi kutikiswa sana.

107 Ilifanya hivyo, kote katika nyakati, mpaka hatimaye kanisa likawazalia Mtoto Mwanamume, na Mtoto huyo Mwanamume alikuwa Neno, Lenyewe, lililofanyika mwili. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu." Yeye alishinda kila pepo, kila nguvu juu ya dunia, iliyompinga, kwa Neno la Baba Yake peke yake. Kila jaribio ambalo Shetani alimpa, Yeye alimkemea Shetani; si kwa ninii Zake—Nguvu Zake Mwenyewe alizokuwa nazo, lakini kwa Neno la Mungu. "Imeandikwa . . . Imeandikwa . . . Imeandikwa . . . " Kwa kuwa Yeye alikuwa ni Neno.

108 Wakati Shetani alipomrukia Hawa, yeye hakuwa Neno, kwa hiyo alishindwa. Wakati alipomrukia Musa, jambo lile lile lilifanyika. Lakini wakati alipomgonga Mwana wa Mungu, Yeye alikuwa na volti elfu kumi. Ziling'oa manyoya yaliyolegea, wakati aliporudi na kusema, "Imeandikwa, 'Mtu hataishi kwa mkate tu, lakini kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu.'" Huyo hapo huyo Mtoto Mwanamume, aliyefanyika mwili. Neno la Milele la Mungu, Mwenyewe, aliyedhihirishwa katika Mwili wa nyama hapa duniani, kuwakilisha Neno.

109 Hivyo ndivyo Yeye alivyojua yale yaliyokuwa katika mioyo yao. Hivyo ndivyo alivyoweza kumwambia Filipo mahali alipokuwa, kwamba yeye alikuwa ni nani. Angeweza kumwambia Simoni Petro alikuwa ni nani. Alimwambia yule mwanamke kisimani. Kwa nini? Yeye alikuwa ni Neno. Kweli. Biblia ilisema, katika Waebrania mlango wa 4, "Neno la Mungu ni kali, lina nguvu kuliko upanga ukatao kuwili, linachoma na kuyagawanya mafuta ya mifupa, na huyatambua mawazo na makusudi ya moyo."

110 Mbona, hao makuhani vipofu wa Kifarisayo hawangeweza kuona kwamba Huyo alikuwa Neno lililodhihirishwa, kwa kuwa walikuwa wamejifungia katika ukuhani na katika mfumo fulani. Na mfumo ule wa kale ilibidi uondoke. Ilikuwa ni Neno, lakini kile kilichoahidiwa kilikuwa kimetimia. Kwa hiyo kama kimetimia, hakina budi kuoza. Ni ganda. Ile Mbegu iliendelea mbele.

111 Musa hangeweza kuleta ujumbe wa Nuhu. Wala Yesu hangeweza kuleta ujumbe wa Nuhu, kwa maana ulikuwa ni wakati mwingine. Na ile mbegu ya kale ilikuwa sawa, lakini ilitimiza kusudi lake na ilikuwa imekufa na kuondoka. Kule kugeuzwa kutoka la kale kuingia kwenye lile jipya, ambapo Uzima ulikuwemo, ndilo jambo lililokuwa likiwatia watu wasiwasi, ndilo bado linalowasumbua siku hizi.

112 Sisi hatujengi ukuta, kama vile tunavyoanza na ujumbe wa Luther, tunaenda moja kwa moja kwenye mstari mnyofu,

ama ujumbe wa Pentekoste. Naami. Tunapiga kona. Tunajenga jengo. Neno la Mungu ndilo ramani. Kila mtu anaweza kujenga mstari ulionyooka, lakini inahitaji mwashi kupiga kona. Inahitaji nguvu za Mungu kufanya jambo hilo. Inahitaji mtu aliyetiwa mafuta kutoka Mbinguni, kutumwa chini kufanya hivyo. Imekuwa hivyo, katika kila wakati. Na katika wakati wa manabii, Neno la Mungu huja kupitia kwa hao manabii, nao wanapiga kona hizo, wakafanya tofauti hizo. Lakini wajenzi walitaka kujenga ukuta. Si ukuta, hata kidogo. Ni jengo, jengo la Mungu.

113 Sasa, tunajisikia na kujua ya kwamba Hii ni Kweli, ya kwamba madhehebu yalioza katika kila wakati. Na kila moja ya madhehebu hayo yalikuwa yameoza na kufa, mpaka ilipozaa hilo Kanisa. Kutokana na machafuko hayo yaliyooza likatoka Neno, Lenyewe. "Neno la Bwana liliwajia manabii." Kamwe halikuja kwa makasisi; lilikuja kwa manabii.

114 Pia angalia, na wakati lilipokuja, hatimaye Neno hilo kwa jumla lilizaliwa hapa katika mwili wa kibinadamu. Utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani Yake. Yeye alikuwa ni Neno. Manabii ni sehemu ya Neno, Neno la wakati wao. Sisi, leo, ni sehemu ya Neno, sisi tunaofuata Neno. Lakini Yeye alikuwa utimilifu wote wa Neno. Alikuwa ni Neno. Yeye alisema . . .

115 Wakati walipokuwa wakimshtaki, akijifanya Mwenyewe sawa na Mungu, maana Yeye alikuwa Mwana wa Mungu, wao walimwambia, "Vema, Wewe unajifanya Mungu."

116 Yeye akasema, "Haikuandikwa katika torati zenu, ya kwamba mnawaita hao ambao Neno la Mungu liliwajia, 'miungu,' wale manabii? Nao walikuwa hivyo. Basi mnawezaje kunihukumu Mimi ninaposema Mimi ni Mwana wa Mungu?"

117 Ambapo, utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili ulikaa ndani ya Mwana wa Mungu. Yeye alikuwa dhihirisho kamilifu la Mungu. Hilo ndilo hatimaye . . . Utungu wa kuzaa chini ya hao manabii, mbona, wao wakiwa ni Neno, walielekeza kwenye huo utimilifu wao wenyewe, utimilifu wa Neno. Na kisha hatimaye taratibu hizo zikafa, mpaka, "Neno likafanyika mwili likakaa kwetu."

118 Angalia jinsi lilivyoonyeshwa katika Yakobo. Angalia jinsi lilivyoonyeshwa katika Yusufu, halisi kabisa. Alipendwa na ndug- . . . baba yake; akachukiwa na ndugu yake, bila sababu. Alikuwa wa kiroho, angeweza kutabiri mambo, na kufasiri ndoto. Hangeweza kujizuia kuwa hivyo. Yeye alizaliwa tu hivyo. Alichaguliwa tangu zamani kuwa hivyo. Lakini, alichukiwa na ndugu zake, na hatimaye akauzwa kwa vipande thelathini vya fedha, karibu vipande thelathini. Kisha akapandishwa cheo, akaketi mkono wa kuume wa Farao. Angalia katika gereza lake, kulikuwako na mnyweshaji na mwokaji; mmoja alipotea na mwingine akaokolewa.

119 Yesu katika gereza Lake, hapo msalabani; mmoja alipotea, mmoja akaokolewa. Barabara kabisa. Kisha akainuliwa hata mbinguni na kuketi juu ya Kiti cha Enzi cha Mungu. Na wakati atakapoondoka tena, kutakuwako na sauti itakayotoka, "Pigeni magoti," na kila ulimi utakiri.

120 Na Yusufu alipoondoka kwenye kiti cha enzi na akaanza kuondoka, tarumbeta ililia, na ilibidi kila goti lipigwe. "Yusufu alikuwa anakuja."

121 Kwa hiyo, siku moja ile Parapanda kuu ya Mungu italia, na waliokufa katika Kristo watafufuka, na kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri Neno hili. Lakini anakuja kutafuta nini? Anakuja hapa kwa ajili gani?

122 Angalia, ilileta hili Neno lililo kamili ambalo lilifanyika mwili, chini ya utungu wa kuzaa wa manabii walionguruma, "Anakuja! Anakuja! Anakuja!"

123 Sasa, lakini ilikuwa bila nabii kwa miaka mia nne, kulingana na historia na Maandiko, kutoka Malaki hadi Yohana. Walikuwa na wanatheolojia tu, makuhani, wachungaji. Sasa hapa tunaweza kuwazia, bila jambo hilo, utaratibu wake ulikuwa umeoza jinsi gani, miaka mia nne bila Ujumbe wa moja kwa moja, wa BWANA ASEMA HIVI, kutoka kwa Mungu. Kwa hiyo, makuhani, manabii, na kadhalika, walikuwa wameiweka katika hali mbaya sana. Ilikuwa imeoza.

124 Basi Yohana, Eliya aliyeahidiwa wa Malaki 3, si Malaki 4. Malaki 3, maana Yesu alinena jambo lile lile katika ninii— katika Mathayo sura ya 11.

125 Wakati jicho la Yohana la tai lilipotiwa utando, kama ninavyoamini kitabu cha Pember kiitwacho *Nyakati za Mwanzoni* kinavyosema. Naye alisema, "Nendeni mkamwulize kama Yeye Ndiye, ama tumtazamie mwingine." Unaona?

126 Naye akasema, Yesu, baada ya kuwarudisha wanafunzi wake, baada ya kuwaambia wakae mkutanoni na kuona kilichotukia. "Nanyi nendeni, mwelezeni Yohana mambo haya. Na heri ni yule asiyechukizwa."

127 Aligeuka na kuwaangalia wanafunzi Wake na watu aliokuwa akiwazungumzia. Akasema, "Mlitoka kwenda kuona nini mlipoenda kumwona Yohana?" Akasema, "Mlienda kumwona mtu aliyevaa mavazi mororo?" Kisha akasema, "Nami nawaambia, hao ni wale wanaokaa katika majumba ya wafalme." Akasema, "Mlitoka kwenda kuona u—u—unyasi uliotikiswa na upepo?"

128 Kwa maneno mengine, kila kitu kidogo kilichozuka, kilimtikisa? "Nitakwambia, kama utakuja tu na kujiunga na kundi letu, tunaweza kukupa mshahara mnono zaidi." Si Yohana. "Kama hutahubiri tu juu ya *hili* na *lile*, vema, unaweza kujiunga na makundi yetu." Si Yohana.

129 Kasema, "Basi mlitoka kwenda kuona nini, nabii? Nami nawaambia, zaidi ya nabii. Kwa kuwa kama mnaweza kulipokea, huyo ndiye aliyenenwa habari zake na nabii, akisema, 'Nitamtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu, kuiandaa njia.'" Hiyo ni Malaki 3:1.

130 Si Malaki 4, hata kidogo. Hiyo ni tofauti. Maana, huyo Eliya akija, ulimwengu utateketezwa mara moja, na wenye haki watatembea juu ya majivu ya waovu.

131 Sasa, angalia. Ujumbe wake haukuwatikisa sana kutokana na usingizi wao wa kidini. Wao walisema tu, "Kuna mtu mwenda wazimu kule chini. Tulikutana naye, karibuni. Alijiita mwenda wazimu; anajaribu kuwazamisha watu kule chini majini. Mnaona? Mbona, mzee huyo hana kitu. Mbona, hata hana mavazi yanayopaswa. Amevaa ngozi ya kondoo. Vema, Yeye ni maskini tu kama bata mzinga wa Ayubu. Mbona, yeye alitoka kwenye seminari gani? Ana kadi ya ushirika gani? Hata hatutashiriki katika mikutano yake. Tutamwacha tu asimame huko chini, afe kwa njaa." Unaona? Ulimwengu haujabadilika sana, wala taratibu. A-ha. "Lakini tutamwacha akae tu sehemu hizo. Hana ninii yo yote . . . "

132 Mnajua ni kwa nini hakufanya hivyo? Kumbukeni, baba yake alikuwa ni kuhani. Lakini kwa nini hakufuata njia ya baba yake, jambo ambalo lilikuwa ndiyo desturi ya watoto kufanya siku hizo? Kwa sababu alikuwa na kitu fulani, Ujumbe mkuu mno. Alikuwa amjulishe Masihi, kwa kuwa Roho Mtakatifu alikuwa amesema hivyo. Hao wachache waliosalia waliokuwa wamerudishwa na Ujumbe wa Gabrieli, sehemu zile, walijua ya kwamba hilo lingekuwa namna hiyo. Kwa hiyo tunaambiwa, akiwa na umri wa kama miaka tisa, alienda jangwani. Baada ya baba yake na mama yake kufa, kwamba alienda nyikani, kwa kuwa ilimbidi asikie sawasawa.

133 Maana, katika lile jengo kubwa mno la kitheolojia kule, wao wangesema, "Sasa, ninajua ya kwamba wewe unapaswa kuwa ndiwe utakayemtangaza Masihi. Isaya alisema ulikuwa unakuja, kwa hiyo utakuwa ile sauti. Sasa, hivi hudhani Ndugu Jones hapa anatimiza masharti hayo barabara?" Naye angeshawishika kwa urahisi.

134 Lakini yeye hakusomea kamwe katika mifumo yo yote yao. Ujumbe wake ulikuwa muhimu mno. Yeye alienda jangwani, kuishi.

135 Angalia. Ujumbe wake haukuwa kama wa mwanatheolojia. Yeye alitumia mifano. Alisema, "Loo, enyi uzao wa nyoka." Akiwaita wale makasisi, "majoka." Hiki, kimojawapo cha mambo mabaya aliyoona nyikani, kimojawapo cha vitu vilivyo na hila, vinavyonyemelea, kilikuwa ni nyoka. Naye akawaza, "Huo ndio hasa mfano mzuri sana wa kulinganisha ninaojua." Akasema, "Enyi uzao wa majoka, ni nani aliyewaonya na

laana ijayo? Msianze kusema, 'Sisi ni wa *hiki* na *kile*,' kwa kuwa Mungu anaweza kutoka katika mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto." "Mawe haya," yale aliyopata nyikani na ufukoni mwa kijito kidogo.

136 "Pia shoka," kitu alichotumia nyikani, "limewekwa kwenye shina la mti," kitu alichoona nyikani. "Kila mti usiozaa matunda mema," anajua mahali alikopata kuni zake, unaona, "hukatwa na kutupwa motoni," alitoa kuni kwake. Mnaona? Ujumbe wake haukuwa wa kasisi, hata kidogo. Ulitokana na maumbile, huko nyikani.

137 Lakini alikuwa na Ujumbe wa kutangaza, naye alikuwa na imani katika Ujumbe wake, kusema, "Yule Masihi, apaswaye kuja, na, hata, Yeye yupo papa hapa miongoni mwenu sasa. Ninawaambia, yupo Mtu anayesimama miongoni mwenu, ambaye hamumjui, ambaye sistahili kuchukua viatu Vyake. Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa Moto."

"Yeye ni nani, Yohana?"

"Mimi sijui."

138 Lakini siku moja, alikuja kijana Mwanamume akienda mtoni, Mtu anayeonekana wa kawaida. Katika ninii tu . . . Mzee Yohana Mbatizaji alikuwa amesimama pale, yule maskini nabii aliyebarikiwa, naye aliangalia ng'ambo ya Yordani. Akasema, "Tazama, yule pale Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu."

"Unamjuaje, Yohana?"

139 "Yeye huko nyikani, aliyeniambia niende nikabatize majini, alisema, 'Yeye utakayemwona akishukiwa na Roho, Huyo ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu.'"

140 Ujumbe wake haungetokana na msimamo wa kitheolojia wala utaratibu uliotungwa na binadamu. Ulibidi uje moja kwa moja kutoka kwa Mungu.

141 Kwa kuwa, Ujumbe wake haukuwatikisa sana. Wao walifikiria, "Loo, yeye alisema aliona hilo. Ninatilia shaka sana. Mimi sioni kitu. Niliangalia. Loo, jamani! Sikuweza kuona kitu juu ya jambo hilo," makuhani na hao wengine walisema.

142 Lakini Yeye alimwona, na tunajua sasa ya kwamba yeye alimwona. Hakika, alimwona. Lakini unaona ulimpata nani?

143 Haukuwatikisa hata kidogo watoke katika usingizi wao. Waliendelea vivyo hivyo, wakakikata kichwa chake, haidhuru. Lakini hau—haukuwashtua.

144 Lakini ulipata wale masalio, wale ambao walikuwa na Uzima ndani yao, lile kundi dogo, Ana na—na Simeoni, na wachache wa hao waliokuwa wakikungoja Kuja kwa Bwana. Naye Ana, huko hekaluni, kipofu, nabii mke aliyemtumikia

Bwana kwa maombi. Halafu siku moja wakati alipokuwa katika Roho . . .

145 Na Simeoni alikuwa ametabiri na kusema, mwanamume mzee, alisema, "Roho Mtakatifu aliniambia ya kwamba sitaona mauti hata nitakapomwona Kristo wa Bwana."

146 Mbona, baadhi ya makuhani, mnajua, walisema, "Maskini mzee yule, yeye kidogo amerukwa na akili, mnajua. Mbona, yeye ameweka mguu mmoja kaburini sasa, na huo mwingine unateleza. Mbona, mwacheni tu. Yeye amekuwa ni mzee wa heshima. Lakini yeye kwa namna fulani . . . "

147 Lakini, unaona, yeye alikuwa na nini? Ilifunuliwa kwake na Roho Mtakatifu.

148 Jambo lilo hilo ndilo lililofunuliwa kwenu ninyi watu alasiri ya leo. Roho Mtakatifu amewaleteni hapa kwa sababu fulani. Baadhi ya ninii . . . Roho Mtakatifu! Angalieni makuhani hawa na makasisi hapa kutoka kwa Wamethodisti, Wabaptisti, Wakatoliki, na kadhalika. Waliongozwa na Roho Mtakatifu. Wakati umewadia. Kwa hiyo Roho Mtakatifu aliwaongoza, nao walikuwa wakimtazamia Huyo, wakiona njaa. Basi, katika ninii tu . . .

149 Siku moja, mnajua, hawakuwa na televisheni. Mungu ashukuriwe kwa ajili ya siku hiyo.

150 Kwa hiyo, wao, walikuwa huko kando ya vilima vya Yuda. M—Mtoto mchanga akazaliwa. Nyota ikatokea, na kadhalika.

151 Lakini baada ya siku nane, mama alimleta yule Mtoto mchanga, amevikwa nguo za kitoto. Ni nguo za kitoto. Ninakwambia . . . nasikia hizo zilikuwa . . . Hawakuwa na nguo za kumfunga nazo. Ilikuwa kidogo ni—kidogo ni kijitambaa kilichotolewa kwenye nira ya maksai, nasikia, hicho ndicho kilikuwa ndio nguo Zake za kitoto. Huyu hapa Yusufu anakuja pamoja na hao wengine, akiingia pamoja na huyu Mtoto mchanga.

152 Ningewazia akina mama walisimama nyuma kwa mbali, wameshika watoto wao na mafulana na kila kitu. Kasema, "Angalieni kule. Unaona? Mnaona? Huyo hapo. Mnaona? Alipewa mimba na yule mwanamume. Huyo hapo anaingia. Huyo, msimkaribie. Kaeni mbali." Wangali wanafikiri namna ile ile.

153 Lakini, Mariamu, akiwa na Mtoto yule mchanga mikononi mwake, hakujali walivyodhani. Yeye alijua huyo alikuwa ni Mwana wa Nani.

154 Na vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwa mwamini ye yote anayelikubali Neno la Mungu moyoni mwake! Sijali yale madhehebu yanachosema. Unajua ni kitu gani. Ni ahadi ya Mungu. Ilifunuliwa kwako na Roho Mtakatifu, wakati ulipotiwa uvuli wa Nguvu Zake. Unajua Kile kinachoendelea. Hakuna

mtu aliye na haki ya kuhubiri Injili mpaka amekutana na Mungu kule nyuma upande wa nyuma wa jangwa katika kile kijiti kinachowaka moto, ambako hakuna shirika la kidini ulimwenguni linaloweza kukuondolea Hilo. Ulikuwapo. Lilitukia kwako. Sijali vile madhehebu yasemavyo. Wewe ni shahidi wake. Haleluya! Ninajisikia kama yule mzee mweusi niliyekuwa nikinena habari zake, "Sina nafasi hapa juu sasa." Unaona? Ninajisikia wa kidini sana wakati huu, ninapowazia. Na hiyo ni kweli. Mungu, Mwenyewe, alikufunulia.

155 Simeoni alikuwa na ahadi. Akiwa ameketi katika chumba chake cha kusomea asubuhi hiyo, loo, nadhani huenda kulikuwako na watoto wachanga mia kadha walioletwa, kila asubuhi. Wayahudi kama milioni mbili na nusu nchini, na watoto hawa wachanga walileta, na wengine wanazaliwa. Kila baada ya siku nane ilimbidi mama aje, kutoa sadaka ya utakaso. Na sasa huyu hapa anakuja . . . Simeoni, ameketi pale, unajua, labda akisoma gombo la Isaya. Sijui. lakini mara . . .

156 Sasa, kama Roho Mtakatifu amekupa ahadi, Roho Mtakatifu hana budi kuitimiza ahadi hiyo, kama kweli Yeye ni Mungu. Yeye, kama Yeye . . .

157 Kama mtu akipita na kusema jambo fulani, Mungu asiliunge mkono, si la Kimaandiko, kwanza. Sahau. Na kama akisema ndivyo ilivyo, na Mungu bado asiliunge mkono, lingali ni kosa.

158 Maana, Mungu hufasiri Ujumbe Wake. Yeye ndiye anayejifasiria. Asemayo yakitimia, ndipo Mungu alisema, "Msikieni, kwa maana ni Kweli." Hilo ni jambo tu la maarifa ya kawaida. Kama akisema litatukia, na linatukia, hilo linalidhihirisha. Halina budi liwe hivyo kila wakati, kuwa ni Kweli kabisa, kwa maana Mungu hasemi uongo.

159 Na kwa hiyo basi huyu hapa Simeoni ameketi pale, akistahimili mateso. Alikuwa masalio. Alikuwa amemsikia Yohana, na masalio machache ya siku zile. Naye huyu hapa ameketi pale, akisikiliza gombo hili, akijua. Ninamaanisha, akijua ya kwamba Yohana alikuwa anakuja, maana yeye—yeye alikuwa ni sehemu ya masalio. Neno lilifunuliwa kwake. Na mara, wakati Mtoto huyo mchanga alipoingia hekaluni, basi ilikuwa ni kazi ya Roho Mtakatifu kufunua ya kwamba Yeye alikuwa pale. Kwa hiyo yeye, akiongozwa na Roho, alitoka kwenye kile chumba kidogo cha kusomea, huyoo moja kwa moja kupitia sebuleni, akafika kwenye huo mstari wa wanawake. Akaja moja kwa moja akiambaa mstari huo wa wanawake mpaka akafika mahali alipokuwa huyu Mtoto Mchanga, wote walikuwa wanamuepa. Akamchukua yule Mtoto mchanga mikononi mwake, akasema, "Bwana, mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani, kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu Wako."

160 Na kwenye wakati huo, mwingine wa hao wachache walioteuliwa katika siku hiyo, alikuwa ni Ana, nabii mke. Alikuwa ameketi hapo, kipofu, pembeni. Akainuka, kipofu. Huyu hapa anakuja, ameongozwa na Roho, kati ya wanawake wote na hao watu waliokuwa wakisongamana ndani na nje ya hekalu, mpaka akaja moja kwa moja akafika mahali Mtoto Kristo alipokuwa.

161 Kama Roho Mtakatifu angaliweza kumwongoza mwanamke kipofu Kwake, vipi kuhusu kundi la Kipentekoste ambao mnapaswa kuwa na macho? Sitaendelea mbele zaidi. Mnajua, kutoka hapo na kuendelea. Angalia. Loo, jamani! Jinsi ambavyo hapana budi kanisa lile lilikuwa kwenye hali hiyo mbaya sana tena, ambayo hakika ilikuwa mbaya, katika siku hiyo! Lakini ulitikisa wale masalio wachache, kama nilivyosema.

162 Sasa hebu na tuwe waaminifu. Kama tukiona kanisa hilo katika hali hiyo leo, je! hivi si tumefikia wakati huo tena? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa hebu angalia tu mambo ya ahadi, za Biblia, ambayo yangekuwa yakiendelea kanisani wakati huu. Tunaona kinachoendelea ulimwenguni, nasi tunaona ni wakati wa mwisho. Sasa hebu na tuangalie kanisani.

163 Hilo, kanisa, lilipata utungu wa kuzaa chini ya Luther. Sasa, tunajua kuna nyakati saba za kanisa, na wajumbe saba kwa hizo nyakati za kanisa, kulingana na Ufunuo. Sasa, wakati ilipobidi Luther aje, bila shaka hilo lilitupa kanisa katika utungu wa kuzaa, lakini lilimzaa Luther. Hiyo ni kweli.

164 Baada ya hayo, likaingia katika shida tena, kwa hiyo likamleta Wesley. Hiyo ni kweli.

Likaenda tena, na likaleta pentekoste.

165 Kila mmoja wa hao wajumbe wa wakati wao, alitikisa sana . . . kurudi kwenye Neno, Ujumbe wa wakati wao, Ujumbe wa kulingana na Biblia. Nina kitabu kinachokuja, juu ya jambo hilo, muhtasari wa milango minne ya kwanza ya Ufunuo. Kisomeni, mara tutakapokichapisha. Na kinathibitisha, bila shaka yo yote, kile ujumbe wa Luther ulichokuwa, kuhesabiwa haki; kwamba utakaso ni nini, hiyo hatua ya pili katika kuzaliwa kwa kawaida. Ndipo wanakuja wapentekoste, sawasawa kabisa.

166 Sasa, angalia, kila wakati ulilitikisa kanisa na kulipa utungu wa kuzaa. Lakini wao walifanya nini? Baada ya utungu wa kuzaa kuja, badala ya kuendelea na Neno, walikusanya kundi la watu pamoja, kama tu lile la kwanza lilivyofanya. Ni kweli kabisa. Mara baada ya kutikiswa na mitume, ndipo tunaliona likikengeuka tena. Ndipo tunaona ya kwamba moja kwa moja wakaja wengi wa hao wengine, Agabo na wengi wa wale watengenezaji huko nyuma katika mwanzo. Kila wakati ulikuwa umefanya hivyo, kama ukisoma kipindi kilichotangulia Baraza la Nikea, Waanzilishi wa Nikea, na huko nyuma kote. Utakuta

yote humo ndani. Kila wakati ulitikiswa, kila wakati mjumbe alipotokea na BWANA ASEMA HIVI.

167 Sasa liko mahali pabaya sana, ambapo, kulingana na Maandiko, kwamba limewahi kuwa hivyo. Tuko katika wakati wa kanisa la Laodikia, "Wakati wa kanisa tajiri, lakini wakati wa kanisa lililo kipofu, ambalo halijui hilo."

168 Hakuna mahali po pote katika Biblia ambapo Kristo aliwahi kutolewa kanisani, ila wakati wa Laodikia. Liko kwenye wakati ulio mbaya sana. Limeoza sana kuliko lilivyopata kuoza. Kasema, "Nimeketi kama malkia, sina haja na kitu."

169 "Nawe hujui ya kwamba wewe ni uchi, mwenye mashaka, kipofu, maskini, wala hujui." Naam, bwana. Kasema, "Nakushauri, njoo ununue Kwangu dawa ya macho, nipate kuyafungua macho yako." Na hilo—hilo bila shaka. . . Dawa ya Mungu ya macho bila shaka italeta Nuru kwa kanisa kama linataka kufungua macho yake kwa yale Mungu aliyosema.

170 Angalia, upesi sasa. Sasa, liko katika hatua hiyo, bila shaka hata kidogo. Tuko katika wakati wa kanisa la Laodikia.

171 Sasa, mjumbe wake ameahidiwa, katika Malaki mlango wa 4. Ameahidiwa kufanya jambo hilo. Na Ujumbe huo ni kwa ajili ya kurudisha Neno, kuwarudisha watu kwenye Neno. Kuzaliwa kutakuwako. Litakombolewa, kwa Kuzaliwa upya, kulingana na Malaki 4.

172 Katika ulimwengu wa kanisa siku hizi, kuna taratibu mbili zinazofanya kazi. Sasa sikilizeni kwa makini sana. Sasa nataka kuona kama mtasema "amina" katika jambo hili. Kuna taratibu mbili zinazofanya kazi katika ulimwengu wa kanisa leo. Nitaondoa jambo hili mgongoni mwangu, na ndipo nilimalize. Sote tunajua ya kwamba hilo ni Neno la Mungu, na utaratibu wa kimadhehebu. Kuna taratibu mbili zinazofanya kazi. Kama tu walivyokuwa, Yakobo na Esau; mmoja kutokana na Roho, mwingine kutokana na mwili. Na ni kitu gani? Esau na Yakobo walikuwa wanapigana katika tumbo la mama, hata wakati walipokuwa wanazaliwa. Na vivyo hivyo madhehebu na Neno, yanapigana, mmoja dhidi ya mwingine. Wamekuwa wakipigana, tangu Luther alipoleta matengenezo ya kwanza. Natumaini hilo ni rahisi vya kutosha hata mnaweza kulielewa. Mnaona?

173 Watu hawa, kama wakichukua *Hili* na kutoka wakaenda Nalo, wanaweza kulielewa zaidi, unaona, kulifikisha mahali ambapo mngeweza. Ninataka tu kuweka Mbegu hii, ndipo ninatumaini wataifanya iwe uhai. Angalia. Unaona?

174 Daima imekuwa namna hiyo. Hiyo ndiyo sababu linapata utungu wa kuzaa, kwa sababu kuna vita ndani yake.

175 Kuna Esau fulani, mtu tu wa ulimwengu, wa kidini sana. Na, loo, yeye ni sawa, mtu mzuri, msafi, mwadilifu, kadiri nijuavyo

mimi, lakini hajui kitu juu ya Haki ya Mzaliwa wa Kwanza. Amezaliwa namna hiyo. Ameumbwa namna hiyo.

176 Na Yakobo, sijali yeye ni nani, yeye anataka hiyo Haki ya Mzaliwa wa Kwanza. Yeye ndiye wa kiroho.

177 Na hao wawili, leo, wako katika tumbo la uzazi wa kanisa. Kuna shirika moja kubwa sana linalojaribu kuundwa, linaloitwa Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Na kutoka katika tumbo la uzazi la kanisa kunatokea watoto wawili. Ninyi zingatieni tu maneno yangu. Ulimwengu una nini hii . . .

178 Neno halina budi kukomboa Kanisa la Bibi-arusi Neno. Kanisa halina budi kuzaliwa kutoka kwake, Bibi-arusi kwa ajili ya Kristo. Hao waliolala katika nyakati zote watamkamilisha huyo Bibi-arusi aliyetoka kwenye Neno walilotoka kwalo, kama vile kutoka kwenye miguu yako hadi kichwani mwako. Anakuwa—anakuwa mkubwa zaidi, na inakubidi kuwa na vya zaidi, na kadhalika. Jinsi huo mwili unavyokua, vivyo hivyo ndivyo nao Mwili wa Kristo unavyokua. Na ndipo hatimaye Kichwa kitakuja kwa Huo, Kichwa hicho Chake, sasa, kama tukiangalia, maana Huo umeninii—wote umeunganishwa na Kichwa. Kichwa ndicho kinachozunguka, kuvuta.

179 Lakini taratibu hizi hazitakua kutokana na Hilo, maana hizo ni taratibu, wala haziwezi kuzaa. Gugu haliwezi kuzaa kishada cha ngano. Lakini zote mbili ziko kwenye shamba moja, wakimwagiliwa maji yale yale, na nuru ile ile ya jua. Moja ni Neno; moja si Neno. Na hizo mbili zinapigana. Zimekuwa zikipigana tangu yale matengenezo ya kwanza, na zingali zinapigana.

180 Sasa, hainibidi kwenda zaidi mbali ya hapo, sivyo? Hakika mnajua ninayomaanisha. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naam, bwana. Haya basi. Haya basi, utaratibu fulani. Je! wewe uko kwenye utaratibu gani?

181 Hebu wazia tu sasa, kama ungaliishi zamani nyuma katika siku hizo za kale, chini ya msukosuko wa manabii wa Mungu na Maneno yaliyotolewa, ungetaka kuwa upande gani katika zamani zile?

182 Vema, una chaguo lile lile leo. Linajitayarisha kuleta Neno lililo kamilifu huko nyuma, nalo Neno linakuja kwa ajili ya Bibi-arusi Neno. Kama vile mwa—mwanamke alivyo sehemu ya mwanamume, ametolewa kwake, vivyo hivyo Kanisa litapaswa kuwa Kanisa linalotii Neno, kila Neno la Biblia; si taratibu, mafundisho ya sharti, wala cho chote kilichoongezwa Kwake. Itabidi liwe ni katika Neno bikira, safi, lisiloghoshiwa. Vema.

183 Na katika siku za Nuru ya Luther, wakati skrubu ya kanisa ilipofungwa, Luther alitumia nguvu. Likaingia katika utungu, lakini yeye akatoka na, "Wenye haki wataishi kwa imani. Na *huu* si ushirika."

184 Sasa, tunaona, ya kwamba, chini ya siku za John Wesley, lilipata utungu tena, lakini kulikuwa—kulikuwa na Wesley aliyezaliwa. Lakini alifanya nini? Alirudi moja kwa moja kama mama yake alivyofanya.

185 Halafu chini ya siku za kipentekoste, baba zenu na mama zenu walitoka kwenye kitu hicho na kukichukia. Walitoka wakaenda mitaani, mama yako akiwa hana stokingi, akipiga-piga mkebe wa kale, na kuzungumza juu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu, na gita la kale. Walilala kwenye barabara za magari, wakalala gerezani usiku kucha. Nasi tu wagumu sana, na tumerudi moja kwa moja kwenye madhehebu na kujifanyia wenyewe takataka ile ile. Waliwavuta watoto wao wakawarudisha kwenye kitu kile kile walichotoka kwake. Wangeshikwa na hamaki kwenye makaburi yao. Wangewaonea aibu. Ninajua hilo ni gumu, lakini ni Kweli. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

186 Mnasema, "Nilifikiri uliwapenda watu." Kama upendo hausahihishi, basi unawezaje kuonyesha upendo? Upendo husahihisha. Nami ninawapenda walimwengu. . . Nina—nina juhudi juu ya kanisa la Mungu.

187 Na kuona taratibu hizi zinazolifunga chini ya mafundisho ya sharti, zikioza. Na Mungu akitangaza kwamba Neno Lake ni Kweli, na bado wanaling'ang'ania. Amina. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni kweli. Unajua ni kweli, ndugu, dada. ["Amina."] Hilo ni Hili tu. Hiyo ndiyo njia rahisi ya kulisema jambo Hilo. Si—si swala la kuchambua Kiyunani, na kadhalika, lakini ni kuvunja-vunja na kuonyesha maana ya kwawaida. Hakika mnaweza kuelewa na jambo Hilo. Mbili na mbili ni nne. Unaona? Sasa tunajua ya kwamba jambo hilo ni kweli.

Sasa, Neno halina budi kumzaa Bibi-arusi.

188 Lakini ule utaratibu wa kale hauna budi kutimiza mfano wake. Hauna budi kumzaa Esau aliyeuza haki zake za mzaliwa wa kwanza.

189 Hili hapa linakuja. Ninalisikia. Natumaini hamfikirii mimi nina kichaa. Lakini kama nina kichaa, niacheni. Ninajisikia vizuri hivi nilivyo. Mimi niko afadhali zaidi namna hii kuliko nilivyokuwa. Na—naweza nikawa na kichaa, kwa ulimwengu. Na—na—najua mahali nilipo. Ninajua mahali ninaposimama.

190 Angalia. Utazaa mtoto mfu, shirika la kidini litakaloyakusanya madhehebu yote pamoja, kumzaa Esau fulani anayemchukia Yakobo. Amina. Natumaini unaona jambo hilo, mtoto aliyezaliwa mfu, madhehebu mafu, yote yakienda pamoja.

191 Loo, enyi waamini wa Neno, upokeeni Ujumbe wangu. Nisikilizeni mimi, si Ujumbe wangu, bali ni Ujumbe Wake ambao Yeye anautangaza kwamba ni Kweli. Huna budi kuchagua kutoka mahali fulani. Huwezi kuketi kimya baada ya jambo hili. Huna budi kujichagulia.

192 Kumbukeni, hivi majuzi, huko sehemu za Westward Ho, asubuhi ile, kwenye kile kifungua kinywa, jinsi Bwana alivyonijalia kuwaonyesha ile ngano? Jinsi ilivyochipuka kupitia kwa Luther, kupitia kwa Wesley, na vishada, na kadhalika, na vitawi vidogo vilivyojitokeza, kila kanisa limewakilishwa katika ghala ya mahindi. Ndipo akaenda moja kwa moja katika ngano hiyo, kama ilivyokuwa kawaida, na kulikuwako na hilo kapi dogo, lililoonekana kabisa kama punje halisi ya ngano. Ukitoka na kuangalia, kama hujui ngano yako, utasema una ngano pale, lakini ni kapi tu. Ndipo unafungua hilo kapi, hakuna ngano mle, hata kidogo. Kule nyuma kabisa, kuna chipukizi dogo la uhai linalochipuka. Hebu chukua darubini uliangalie. Na wakati Pentekoste ilipotokea kwa mara ya kwanza, ilifanana sana, Yesu alisema katika Mathayo 24:24, "Ingewapoteza walio wateule kama yamkini." Ilikuwa ifanye nini? Isaidie punje. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa, kishada . . .

193 Angalia hapa. Hilo jani halifanani na punje iliyoanguka, wala kishada, lakini hufanana zaidi Nayo. Na kapi linafanana sana nayo, lakini bado si ngano. Ni mbebaji wa ngano.

194 Je! huoni jinsi jumbe hizo zilivyokuja pamoja na utungu wa kuzaa? Lakini Uhai uliondoka moja kwa moja mle, upate kwenda kwenye ujumbe uliofuata. Uhai ulitoka moja kwa moja kutoka kwa Luther, ukaingia katika ujumbe wa Wesley. Moja kwa moja kutoka ujumbe wa Wesley, ukaingia katika ujumbe wa kipentekoste. Sasa wakati umewadia tena, kuliacha kapi. Kuna nini? Hayo hapo maumbile, katika kila hali, yakitangaza kwamba hiyo ni Kweli.

195 Sasa mnaona ni kwa nini mnafikiri mimi ni mkichaa. Labda niko hivyo, kama nilivyosema. Lakini kuna Kitu fulani ndani yangu. Siwezi kukinyamazisha. Hasha, sikuwahi kukiweka humo ndani. Mimi sikujichagulia. Ni Mungu. Naye anathibitisha jambo Hilo, kuthibitisha ya kwamba ni Kweli, kulifanya kuwa ni Kweli. Si kwamba eti nina jambo lo lote dhidi ya Luther, na Wesley, Wapentekoste, ama Wabaptisti, ama wo wote wale. Sina neno dhidi ya mtu ye yote. Mimi ninapinga hizo taratibu, kwa kuwa Neno linazipinga; si watu. Angalia hawa mapadre na makasisi wanaoketi hapa, leo. Wasingekuwa hapa kama walisikiliza madhehebu yao, lakini walikuwa na ujasiri wa kawaida, wa Neno la Mungu, wa kutoka nje na kulikubali. *Haleluya* linamaanisha "Mungu wetu asifiwe." Halitawadhuru. [Mtu fulani anasema, "Amina."—Mh.] Linamaanisha "na iwe hivyo." Ninaamini jambo hilo. Ninaamini na ninajua ya kwamba ni Kweli. Imethibitishwa kuwa ni Kweli. Siku moja mtaona, labda itakuwa mmechelewa sana. Sasa angalieni. Angalieni.

196 Biblia ilisema, "Mkewe amejifanya tayari," mwishoni mwa wakati. Yeye alijifanya tayari vipi? Kuwa Mke Wake. Naye anafanya nini? Alikuwa amevaa vazi la namna gani? Neno Lake

Mwenyewe. Alikuwa amevaa Haki Yake. Ndiyo hivyo. Ni kweli. Unaona?

197 Ono! Angalia, ninafunga tu sasa hivi. Ninataka kusema jambo hili moja kabla tu sijafunga. Hilo ndilo lililonifanya kusema jambo hili. Sasa, ni BWANA ASEMA HIVI. Mtu angetamka hivyo, bila, kuliweka katika mawazo yake mwenyewe, angekuwa mnafiki na angepaswa kwenda jehanamu kwa ajili ya jambo hilo. Ni kweli. Kama angejaribu kupata kundi la watu, watu wazuri kama hawa, na kuwadanganya, mbona, yeye angekuwa ibilisi katika mwili. Mungu hangemheshimu kamwe. Unafikiri Mungu angemheshimu ibilisi au uongo? Hata kidogo. Unaona? Linapita juu ya vichwa vyao, wala hawalipati. Yeye anawavuta Wateule kuwatoa nje.

198 Angalia manabii wote kote katika zile nyakati, jinsi alivyowapata Wateule.

199 Angalia, wakishuka kuja, hata kwenye yale matengenezo. Kama vile, kanisa la Katoliki la Kirumi lilivyomchoma moto Joan wa Arc, eti ni mchawi. Hiyo ni kweli. Baadaye wakaona kwamba hakuwa mchawi. Alikuwa ni mtakatifu. Bila shaka, walifanya vitubio, wakaichimbua miili ya hao mapadre na kuitupa mtoni. Lakini, unajua, lakini hilo halikutatua mambo katika vitabu vya Mungu. La. Walimwita Mtakatifu Patrick hivyo, pia, unaona, na basi kama mimi ni mchawi yeye naye ni mchawi pia. Kwa hiyo, tunaona, angalia watoto wake. Angalia mahali pake, juu, angalia aliwaua wangapi. Angalia kwenye orodha ya wafia imani uone ni wangapi waliouawa pale. Unaona, sivyo ilivyo.

200 Lakini madai ya watu, hilo halilifanyi jambo hilo kuwa hivyo. Ni kile Mungu alichosema na kuthibitisha, kwamba ni kweli. "Thibitisha mambo yote. Shikilia sana yaliyo mema."

201 Sasa tunaona, sasa, hapa yapata miezi michache iliyopita, asubuhi moja, nilikuwa nikitoka nyumbani, ndipo ono likatokea.

202 Nami ninamsai mtu ye yote hapa, ambaye amejua miaka hii yote, akaseme wakati wo wote ambapo Bwana aliwahi kuniambia "BWANA ASEMA HIVI" ila jambo hilo lilitukia. Ni wangapi wanaojua kwamba ni Kweli, inua mkono wako. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kweli. Mtu ye yote angeweza kusema vinginevyo? [Ndugu Branham anatulia. Kusanyiko linanyamaza.] Ni kweli.

203 Usimjali mjumbe. Angalia kwamba Ujumbe ni nini. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni huo Ujumbe. Unaona? Si yeye. Usiangalie huyo ninii mdogo [Sehemu tupu kwenye kanda.] mwenye upara, unajua, mtu, maana ni ninii— ni mwanadamu tu, wote, na sisi sote tu sawa tu. Lakini angalia jambo linalotendeka. Hilo ndilo linalolitangaza. Nilichukuliwa . . .

204 Sasa, ninajua watu husema mambo ya kila namna, na tunajua ya kwamba mengi ya hayo si kweli. Siwezi kuwajibika kwa yale hao wengine, mtu ye yote asemayo. Sina budi kuwajibika kwa yale nisemayo mimi. Ninaweza tu kusema kama ni Kweli, ama la. Nami ni—ni—ndimi ninayepaswa kuwajibika kwa jambo hilo, si yale mtu mwingine anayosema. Siwezi kumhukumu mtu ye yote. Sikutumwa kuhukumu, bali kuhubiri Ujumbe. Angalia.

205 Nilikuwa ni—nionyeshwe Kanisa hapo kabla. Nami nilichukuliwa na Mtu fulani ambaye sikuweza kumwona, nami niliwekwa mahali pa juu, kama vile, kwenye jukwaa. Ndipo nikasikia muziki mtamu sana niliopata kusikia. Basi nikaangalia, wanakuja, na kundi la wanawali, yapata, walionekana kama, loo, wenye umri wa miaka kama ishirini, kumi na nane, ishirini. Na wote walikuwa na nywele ndefu, na walikuwa wamevalia mavazi tofauti, mfano, mavazi. Nao walikuwa wakienda kwa utaratibu kwa hatua kamilifu, kwa muziki huo, walivyoweza. Nao wakaenda kutoka kushoto kwangu, wakizunguka namna *hii*. Nami nikawaangalia. Nami nikaangalia basi kuona ni nani aliyekuwa akinena nami, wala sikuweza kumwona mtu ye yote.

206 Baadaye nikasikia bendi la roki likija. Nami nilipoangalia upande wangu wa kulia, wakija namna *hii*, wakirudi, haya hapa makanisa ya ulimwengu yanakuja. Na baadhi ya . . . Kila moja likibeba bendera zao, za kule walikotoka. Baadhi ya vitu vichafu sana nilivyopata kuona maishani mwangu! Na wakati kanisa la Marekani lilipotokea, lilikuwa ndilo baya sana nililopata kuona. Baba wa Mbinguni ndiye shahidi wangu. Walikuwa wamevaa sketi hizi chafu sana za kijivu, kama mmoja wa hawa wasichana wa baa, zilizo tupu upande wa nyuma, hapa *juu;* wameshikilia kitu kinachoonekana kama kipande cha karatasi ya kijivu; na kama dansi la hula; wamejipaka rangi; wamevaa kaptura fupi, wamekata nywele; wanavuta sigara; na wakikatika viuno, huku wakitembea kwa mdundo wa roki.

Nami nikasema, "Je! hilo ndilo kanisa la Marekani?"

Na ile Sauti ikasema, "Naam, ndilo."

207 Nao walipopita, iliwabidi kukishikilia namna *hii*, na kuiweka ile karatasi nyuma yao walipopita.

208 Ni—nikaanza kulia. Ni—nikawazia tu, "Juhudi yangu yote, na yote niliyofanya." Na kila kitu ambacho sisi wahudumu tumefanya pamoja . . . Na, enyi ndugu, si—sijui mnaweza kuamini maono haya kiasi gani; lakini ni Kweli, kwangu mimi. Daima imethibitika kwamba ni kweli. Nilipoona jambo hilo, na nikijua jambo lililokuwa linaendelea, moyo wangu ulikuwa karibu kupasuka ndani yangu. "Nimefanya nini? Nimelikosaje? Nimedumu sawasawa na hilo Neno, Bwana. Na ningewezaje kufanya jambo hilo?"

209 Niliwazia, "Ungewezaje Wewe kunipa ono, si muda mrefu uliopita, na kuniona Humo? Na kusema, 'Vema, je! itawabidi wao kuhukumiwa?' Yeye akasema, 'Kundi la Paulo, pia.' Nikasema, 'Nimehubiri Neno lile lile yeye alilohubiri.'" Wafanyabiashara Wakristo waliandika makala hayo. Nami nikasema, "Kwa nini? Kwa nini iwe hivi?"

210 Niliona lile kundi la malaya likipita namna hiyo, wote wamevalia namna hiyo, na kujiita, "Kanisa la Bi Marekani." Ni—nilizimia tu.

211 Halafu, moja kwa moja, nikasikia ule muziki mtamu sana ukija tena, na huyu hapa maskini yule Bibi-arusi mwanamwali anapita tena. Yeye akasema, "Huyu ndiye anayetokea, hata hivyo." Na wakati alipopita, Yeye alikuwa anafanana kabisa na Yule aliyepita mara ya kwanza, akitembea kwa hatua ya muziki wa Neno la Mungu, akitembea kijeshi. Na wakati nilipoona jambo hilo, nilisimama pale huku nimeinua mikono yangu, nikilia, namna *hiyo*. Nilipopata kujirudia, nilikuwa nimesimama nje kule kwenye ukumbi wangu, nikiangalia upande wa pili wa uwanja.

212 Ni kitu gani? Yeye anapaswa kuwa Bibi-arusi yule yule, wa namna ile ile, ameumbwa kwa vitu vile vile Huyo alivyoumbwa navyo mara ya kwanza. Sasa soma Malaki 4 na uone kama hatupaswi kuwa na Ujumbe katika siku za mwisho, ambao "utaigeuza mioyo ya watoto iwaelekee baba zao," kurudi kwenye Ujumbe wa pentekoste ya kwanza, Neno kwa Neno. Ndugu, tumewasili.

213 Sasa, kanisa hili linapaswa kupata ishara, na ni ishara ya mwisho. Tunaona hapa ya kwamba, katika—katika—katika Maandiko, unaona sasa, unaona, ule utungu mkuu wa kuzaa ulio katika wakati huu wa Laodikia. Unachosha. Kanisa lao linazaliwa mara ya pili. Si . . .

214 Hakutakuwako na madhehebu mengine. Kila mtu anajua ya kwamba kila wakati ujumbe ulipotoka . . . Waulize hawa wanahistoria. Baada ya ujumbe kutolewa, madhehebu yalitokea kwake; loo, Alexander Campbell, cho chote kile, Martin Luther, na kila kitu. Waliunda madhehebu kutoka kwake. Na kwa kawaida ujumbe huendelea kwa miaka mitatu tu hivi, uamsho. Huu umekuwa ukiendelea kwa miaka kumi na mitano, wala hapakuwa na madhehebu yaliyotoka kwake. Kwa nini? Kapi lilikuwa ndilo la mwisho. Tuko katika wakati wa mwisho.

215 Unaona utungu wa kuzaa? Unaona kuna nini? Masalio tu ndiyo yatakayotolewa. Masalio tu ndiyo yatakayotolewa. Na hiyo ndiyo sababu ninalia, na kukazana, na kusukuma, na kuweka kando kila upendeleo wa mwanadamu duniani, nipate kibali cha Mungu, na kuendelea tu katika Neno Lake.

216 Iko katika utungu. Hiyo ndiyo shida yake. Itazaa. Haina budi kujichagulia. Maandiko ya mkono yapo ukutani. Tunaona

ulimwengu uko karibu kuangamia. Hiyo ni kweli. Na tunaona kanisa, limeoza sana, liko tayari kuangamia. Na utungu wa kuzaa uko sehemu zote, kwenye ulimwengu na juu ya kanisa.

217 Na ulimwengu mpya uko karibu kuzaliwa, na Kanisa jipya kuzaliwa, lipate kwenda kwake, kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu. Tunajua jambo hilo.

218 Angalia. Mungu analipa . . . Na sikilizeni jambo hili kwa makini, ndipo nitafunga. Ishara yake ya mwisho; Ujumbe wake wa mwisho; Ishara yake ya mwisho. Ishara yake ya mwisho, ni, halina budi kuingia katika hali lililokuwamo hapo mwanzo; ulimwengu, kanisa.

219 Angalia jinsi ilivyokuwa hapo mwanzo, miaka hiyo yote, bila, kutoka Malaki mpaka Yesu. Angalia jambo hilo, miaka hiyo yote sasa. Liangalie, huko nyuma kote, walivyoingia kwenye upotovu. Angalia dunia, jinsi ilivyokuwa kila wakati, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, kadhalika. Haina budi kuwa ni aina ile ile ama mfano, nasi tunaona jambo hilo. "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Tunaona mambo haya yote yakifanana tu.

220 Halafu, tunapata ishara moja ya mwisho. Katika Luka, mlango wa 17, kifungu cha 28, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Kwa kuwa, kama ilivyokuwa katika Sodoma, unaona. Sasa, Yesu alisoma Biblia ii hii, Kitabu cha Mwanzo kile kile tunachosoma. Sasa, kwa makini, usilikose. Biblia ii hii tunayosoma, Yesu aliisoma. Naye aliliambia Kanisa Lake, "Angalieni mwone wakati siku za Sodoma zitakaporudi tena," watu waliopotoka, wanaume wakipoteza ninii yao ya asili.

221 Angalia ulawiti, jinsi unavyoongezeka ulimwenguni siku hizi, katika gazeti hivi karibuni tu. Unapaswa kuingia katika ofisi yangu na kusoma barua kutoka kwa akina mama, kwa ajili ya wavulana wao. Na ulawiti unaongezeka kwa, nafikiri, ni asilimia ishirini ama thelathini katika—katika California, peke yake, mwaka jana. Kundi kubwa la . . . la hata watu wa serikali, wamethibitisha kwamba wao ni walawiti. Ninyi watu wa serikali mnajua jambo hilo. Magazeti yenu, niliyasoma, na katika mambo mbalimbali yaliyotukia. Kama ukininii . . .

222 [Dada fulani ananena kwa lugha nyingine, na halafu anafasiri. Dada yuyo huyo tena ananena kwa lugha nyingine, na halafu tena anafasiri. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

223 Nina ufahamu mzuri wa Maandiko. Hivyo ndivyo hasa Mungu alivyosema ingetendeka. "Yeye anenaye katika lugha pia na aombe apate kufasiri."

224 Hiyo ni kweli. Nimewaambia Kweli, basi Mungu yupo hapa, akithibitisha jambo Hilo. Ni Kweli. Hiyo ni kweli.

225 Sasa angalia. Ujumbe huo wa mwisho ambao Yesu aliusema ulikuwa ni nini? "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma," angalia sasa, kabla tu ulimwengu wa Mataifa kuteketezwa, huo moto. Sasa jaribuni kuelewa. Ni jambo gani lililotukia? Kulikuwa na kundi la watu, wafuasi vuguvugu wa kanisa, kama Lutu na kundi lake kule Sodoma. Kulikuwako na mtu mwingine ambaye alikuwa tayari ametoka ndani yake. Hakuwa ndani yake, kwanza. Huyo alikuwa ni Ibrahimu, yule aliyekuwa na ahadi ya kuja kwa mwana. Mnaelewa? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema.

226 Na, sasa, kabla tu ya kufikia kile kilele cha yale maangamizi, Mungu alimtokea Ibrahimu katika sura nyingi, lakini wakati huu Yeye alitokea kama Mwanadamu. Yeye alikuwa Mwanadamu. Ndipo akamsogelea Mungu.

Sasa, unasema, "Haikuwa ni mwanadamu."

227 I—I—I—Ilikuwa ni Mungu ndani ya yule Mwanadamu. Ibrahimu alimwita, "Elohimu." Alikuwa ni Mtu.

228 Na, angalia, Yeye aliketi chini, huku mgongo Wake umeelekea kwenye hema, kisha akasema, "Yupo wapi Sara, mkeo?"

Kasema, "Yumo hemani, nyuma Yako."

229 Kasema, "Nitakuzuru wakati huu mwakani, ambapo nilikuahidi." Ndipo Sara akacheka. Naye akasema, "Kwa nini Sara amecheka?" Unaona?

230 Sasa, hilo ndilo lililokuwa linaendelea katika siku ile. Kuonyesha tu ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu aliona, kundi la Walioteuliwa likitolewa, kutoka Sodoma. Sasa, usikose mfano huu, hata iweje. Kundi lililokuwa limetolewa, ambalo kwanza, halikuwa Sodoma.

231 Lakini Malaika wawili kati ya hao wakashuka wakaenda Sodoma. Na wakati walipofika huko, tunamwona Lutu. Naye akamkuta katika hali ya kuanguka, walawiti wote na upotovu. Mnajua hadithi hiyo.

Lakini kuna mmoja aliyebaki na Ibrahimu, ambaye alikuwa ni Elohimu.

232 Wao walihubiri Neno kule. Kuhubiri Neno kuliwapofusha, wala hawangeweza kuuona mlango. Hivyo ndivyo ilivyo leo.

233 Lakini Yule aliyekuwa pamoja na kundi lililotoka, alifanya muujiza mbele ya Ibrahimu, kuonyesha kwamba yeye alikuwa ni nani, naye alikuwa pamoja na Ibrahimu.

234 Akasema, "Kwa nini Sara amecheka?" Kuhusu huyu mtoto mchanga. Ndipo Sara akatoka akasema hakucheka. Ndipo akasema, "Lakini ulicheka." Naye angalimwua papo hapo kama yeye hangekuwa sehemu ya Ibrahimu.

235 Vivyo hivyo Mungu angeweza kutuua kama hatungekuwa sehemu ya Kristo. Rehema ya Kristo inatushikilia kabisa, sisi wenye kushuku na upotovu katika Neno.

236 Lakini, angalia, angalia jambo lililotukia. Yesu anageuka sasa, na kusema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika wakati wa mwisho wakati Mwana wa Adamu atakapoanza kujifunua Mwenyewe." [Sehemu tupu katika kanda—Mh.] Unaona? "Mwana wa Adamu" daima, katika Biblia, ni *nabii*. Unaona? Yeye alikuja katika Majina matatu ya mwana: Mwana wa Adamu, Mwana wa Mungu, Mwana wa Daudi. Unaona? Naye alitamka Jina Lake, "Mwana wa Adamu," kwa sababu hiyo ndiyo kazi aliyofanya, ya nabii, mwonaji. Yeye alisema, "Katika siku kama ilivyokuwa katika Nuhu, wakati Mwana wa Adamu atakapoanza kujifunua Mwenyewe, huo utakuwa ni wakati wa mwisho."

237 Sasa hebu na tuwazie tu, kwa dakika moja tu. Kamwe ulimwengu haujapata mjumbe kote ulimwenguni. Tumekuwa na akina Finney, Sankey, Moody, Finny, Knox, Kalvini, na kadhalika, kote ulimwenguni, wajumbe kwa kanisa katika utungu huu wa kuzaa. Lakini kamwe hatujapata mtu akitoka kwenda akiwa na ujumbe wa kimataifa, mpaka siku hii, mwenye jina linaloishia katika h-a-m. A-b-r-a-h-a-m, lenye herufi sita . . . A-b-r-a-h-a-m ni herufi saba.

238 Tuna mtu mmoja leo anayeitwa G-r-a-h-a-m, herufi sita, na sita ni namba ya ulimwengu, siku ya kuumba. Ni lini ulimwengu ulipata kuwa na mtu ndani yake sasa, akihubiri katika *ulimwengu*, kule ulimwenguni, kule chini akiwaita watu watoke, "Tubuni, tubuni!, Mtaangamia, iwapo hamtatoka kwake," mpaka wakati huu? G-r-a-h-a-m, angalia analofanya, anahubiri Neno, akiwapofusha watu walio nje, akiita, "Tokeni," mjumbe kutoka kwa Mungu. Yesu alisema hilo lingetukia wakati tu ambapo Mwana wa Adamu atakapojifunua Mwenyewe. Sasa, hilo, hilo litakuwa wapi? Huko nje kwenye utaratibu wa kanisa, ulimwengu. Nao wakaanza kumchukia huyo mtu, kwa ajili ya jambo hilo.

239 Lakini, kumbukeni, kulikuwako na kundi fulani, pia, ambalo lilikuwa ni kundi la kiroho, lile kundi la Yakobo, si—si kundi la Esau. Kulikuwako na kundi la Yakobo lililokuwa likimtazamia mwana, ambalo halikuwa katika hiyo Babeli, nao walipokea Mjumbe. Mnaelewa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Abraham, A-b-r-a-h-a-m, walipokea Mjumbe. Na huyo Mjumbe, ni jambo gani kuu, la ajabu, alilofanya Yeye, kuonyesha ya kwamba ilikuwa ni mwisho wa wakati? Alitambua mawazo yaliyokuwa katika moyo wa Sara.

240 Naye Yesu, Mwana wa Mungu, aliyefanyika mwili, akionyesha ya kwamba Roho wa Mungu angerudi kwenye Kundi hilo dogo lililoteuliwa kwenye wakati wa mwisho, naye

angejifunua Mwenyewe katika hali ile ile. Utungu wa kuzaa! Loo, ndugu, tafadhali jaribu kuelewa. Jaribu sana. Fungueni mioyo yenu kwa dakika moja. Mwangalie Kristo. Mungu yeye yule yuko hapa sasa hivi. Yeye Yule. Aliahidi mambo haya. Na kama Yeye aliyaahidi, bila shaka Yeye anaweza kuyafanya.

241 Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Nawatakeni ninyi muwazie tu, kwa kicho.

242 Baba, liko mikononi Mwako sasa. Nimefanya yote niwezayo kufanya. Ninaomba ya kwamba utawasaidia watu ku—kufahamu. Mbegu imekwisha kupandwa. Imwagie maji, Roho, juu Yake, Bwana, na uimwagilie maji kwa ajili ya Utukufu Wako. Kama nilifanya kosa, Bwana, sikumaanisha kufanya jambo hilo. Ninaomba, Mungu, ya kwamba—ya kwamba utalifasiri vizuri, kwenye mioyo yao, kusudi waweze kuona na kufahamu. Tujalie, Bwana. Katika Jina la Yesu, naomba. Amina.

243 Bwana awabariki. Ninawapenda. Mungu huyu aliyehubiri Neno hili, Mungu huyu ambaye anawajibika kwa Neno hili . . . Mimi ninahusika tu katika kulisema. Yeye ndiye anayepaswa kulihuisha. Mungu yuyo huyo yuko hapa.

244 Sasa, ni wangapi huko nje walio na haja? Inua mkono wako. Je! Yeye aliahidi kufanya mambo haya katika siku za mwisho? Sasa niangalieni. Sasa ni kama Petro na Yohana walivyosema, "Tuangalie sisi." Kama kwamba . . . Mnaona? Yeye aliwaambia. Sasa ninyi angalieni huku. Sasa, tafadhali msisogee hapa na pale. Huu ni ninii sana . . . Nina—ninajaribu, moyo wangu wote ndani yangu. Iweni tu na uchaji. Mnaona? Kila mmoja wenu, ni roho, mnapotembea. Bila shaka, wewe ni kitu kizima. Ninajaribu kushika imani ya watu hawa.

245 Maskini mwanamke fulani alipita na kugusa vazi Lake, akaondoka akaenda akaketi. Yesu alimwambia shida yake ilikuwa ni nini, naye akaponywa.

246 Na sasa Yeye aliahidi kufanya jambo hilo tena, Mwana wa Adamu atajifunua tena kama alivyofanya huko Sodoma. Ulimwengu uko katika hali hiyo. Kanisa limo katika hali hiyo. Sasa je! Mungu ametimiza Neno Lake? Angalia kama amelitimiza, ama hajalitimiza. Loo, tumekuwa na ishara nyingi, kuruka, kunena kwa lugha, unabii, na kadhalika. Lakini, hebu ngoja, kuna ishara nyingine. Loo, tuna kuigiza kwingi kimwili. Hilo linalifanya tu lililo halisi kunawiri. Dola yoyote ya bandia inapaswa kuitanya iliyo halisi kunawiri.

247 Sasa ninyi ombeni. Amininі. Ninii tu, na—nawasai kufanya jambo hilo. Ninyi angalieni, na aminini yale niliyowaambia. Ni wangapi wanaoamini jambo hili kuwa ni Kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sijali wewe ni nani, mahali ulipo. Nitaninii tu . . .

248 Kila mtu hapa, nijuavyo mimi, ni mgeni kabisa, ila Bill Dauch na mkewe wanaoketi papo hapo, nijuavyo mimi. Nafikiri

ninamjua maskini mhubiri huyu kutoka Ujerumani, anayeketi papo hapo. Na, ndugu, na watu wawili watatu wanaoketi pale pale.

249 Mtu fulani kule nyuma katika wasikilizaji, angalia, kule nyuma kabisa. Ninawasai kuamini yale niliyowaambia ni Kweli.

250 Vipi wakati yule Malaika wa Bwana aliposhuka mtoni kule, miaka thelathini na mitatu iliyopita, na kutoa tamshi hili? Nilijuaje?

251 Na mchungaji wangu mwenyewe wa Kibaptisti alinifukuza kanisani, kasema, "U—ulishikwa na jinamizi, Billy."

252 Nikasema, "Jinamizi, hata kidogo, Dk. Davis. Hivyo ndivyo wewe, msimamo unaochukua, hata afadhali uchukue kadi yangu ya ushirika."

253 Nilijua kutakuwako na mtu fulani, mahali fulani, ambaye angeamini jambo hilo. Mungu asingetuma Ujumbe isipokuwa pawe na mtu wa kuupokea.

254 Loo, hakika, nilipotoka kwenda kuwaombea wagonjwa, lilikuwa ni jambo zuri sana. Lakini wakati nilipoanza kuwaambieni Kweli ya Neno, mambo yamekuwa vingine. Mnapaswa kujua. Kila Ujumbe umekuwa namna hiyo.

255 Yesu alikuwa mzuri sana wakati alipokwenda kanisani na kuwaponya watu, na kila kitu. Lakini wakati alipoketi chini siku moja, na kusema, "Mimi na Baba Yangu ni mmoja," loo, hilo, hilo lilitosha. "Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna Uzima ndani yenu." Hakueleza Hilo. Alitaka kuona ni nani angalisimama upande Wake. Sawa.

256 Unaonaje, ku—kundi likiwa na madaktari na kadhalika, liseme, "Mtu huyo ni . . . Mbona, Yeye ni mnyonya damu. Ati tuule mwili Wake na kuinywa Damu Yake?" Yeye hakulielezea Hilo hata kidogo. Hakulielezea.

257 Lakini, hata hivyo, Neno hilo lilikuwa limeshikilia, kwa hao mitume. Hawakujali. Hawakulifahamu. Waliliamini, hata hivyo. Unaona? Walijua, maana walikuwa wameona kazi za Mungu, nao walijua ilikuwa hivyo. Yeye alisema, "Hizo ndizo zinazonishuhudia Mimi."

258 Huyu hapa mtu fulani, mwanamke ameketi papa hapa, ameinua mkono wake juu. Sasa, mnaweza kuniita mshupavu wa dini, mkitaka; lakini Nguzo ile ile ya Moto, iliyowaongoza wana wa Israeli katika jangwa, iko moja kwa moja juu ya mwanamke yule.

259 Sasa, kumbukeni, Yesu alisema, "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo ninyi mtaniona. Nilitoka kwa Mungu. Ninarudi kwa Mungu," baada ya mauti Yake, kuzikwa. Yeye aliwaambia Wayahudi. Alisema, "Mimi . . . "

260 Yeye alikuwa ni ule Mwamba uliokuwa jangwani. Alikuwa ni ile Nguzo ya Moto, "MIMI NIKO AMBAYE NIKO." "MIMI NIKO" alikuwa nani? Ile Nguzo ya Moto katika kile kijiti kilichowaka moto. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naye alifanyika mwili akakaa kwetu. Kasema, "Nilitoka kwa Mungu, na ninarudi kwa Mungu, kusudi arudi katika umbo la Roho Mtakatifu."

261 Na Yeye yuko hapa, pamoja nasi leo, Yeye amepigwa picha za kisayansi. Huyu hapa, kuthibitisha zaidi ya picha yo yote ya kisayansi, cho chote. Yuko hapa, kuthibitisha jambo hilo, kwa kuwa ni Yeye. "Mimi Mwana wa Adamu nitafunuliwa katika siku hii." Sasa, *yule* pale. Ninamtazama moja kwa moja.

262 Unasema, "Je! unaiona?" Yohana aliiona, pia, lakini hao wengine hawakuiona.

263 Angalia, kuthibitisha jambo hilo sasa. Mwanamke yule ni mgeni kwangu. Sijapata kumwona—kumwona, maishani mwangu. Lakini ana kasoro fulani katika mojawapo ya viungo vyake ambavyo anaombea. Ni . . . Hiyo ni kweli, mama. Ulifanyiwa upasuaji. Huyu anayeketi kando yako ni mumeo. Hutoki hapa. Umetoka California. Jina lako ni Roland. Shida yako ya tumbo imekwisha, pia, bwana. Ulikuwa na shida ya tumbo. Sivyo? Vema, imekwisha kabisa. Mguu wako umeponywa.

"Katika siku hiyo Mwana wa Adamu . . . "

264 Hapa, kuna mtu anayeketi moja kwa moja *hapa*, mwanamume yule pale. Ni mtu mweusi, ana kasoro katika macho yake. Yeye ni ninii . . . Naam. Yeye, kazi afanyayo, yeye hufanya jambo fulani kuhusu motokaa, huosha motokaa, mwosha magari. Vema. Macho yako yanaharibika. Ndiyo kwanza uamini, sivyo? Jambo fulani la ajabu lilikupata. Jina lako ni Fred. Hiyo ni kweli. Jina lako la mwisho ni Conn. Hiyo ni kweli. Unaamini sasa? Macho yako hayatakusumbua tena basi. Sijawahi kumwona mtu huyo, maishani mwangu.

265 Mwanamume aliyeko huko nyuma kabisa kule, wala yeye hatoki hapa. Anatoka California. Ana mgongo mbaya, Bw. Owens. Huyo ni wewe. Bwana Yesu anakuponya. Sijawahi kumwona mtu huyo, maishani mwangu, sijui kitu juu yake. Ninafuata tu ile Nuru inavyokwenda.

266 "Ukiweza kuamini, mambo yote yanawezekana kwao hao waaminio."

267 Jamaa huyu mdogo anayeketi hapa, ana ugonjwa wa ngiri, amevaa miwani na suti ya kijivu. Fred, Mungu anakuponya kama ukiamini hilo. Utalikubali? Vema. Sijapata kumwona, maishani mwangu.

268 Bibi Holden, unayeketi kule kutoka kwake, unayeumwa na macho. Mimi simjui mwanamke huyo, sijapata kumwona

maishani mwangu, lakini hilo ni kweli. Unaona? "Kama unaweza kuamini."

269 Unalia nini, dada? Una ugonjwa wa kuchanganyikiwa, vidonda kooni, ugonjwa wa moyo. Unaamini kwamba Mungu atakuponya? Unayeketi mwisho wa kiti pale. Kama unaamini, kwa moyo wako wote, Yesu Kristo atakuponya. Wasiwasi huo wote utakuondoka, unajisikia kama kwamba umerudi katika hali yako njema. Ibilisi anakuambia uongo. Unakubali jambo hilo? Sasa inua mkono wako, useme, "Nitalikubali, basi." Sawa. Yote yamekwisha.

270 Ni kitu gani? Kanisa linapitia katika utungu wa kuzaa. Je! utafanya uamuzi wako sasa katika Uwepo Wake? Nimewaonyesha Neno hasa, yale aliyosema angefanya.

271 Tafuteni katika jengo hili, mwulizeni mtu ye yote ambaye hata amewahi kuguswa, ama kuzungumziwa, ama cho chote kile kilichofanyika, mwone kama nimepata kuwaona, kuwajua, ama jambo lo lote juu yao. Mnafikiri mwanadamu angaliweza kufanya jambo hilo? Hilo haliwezekani kabisa kwa jambo hilo kutukia.

272 Vema, ni Kitu gani? Mwana wa Adamu. "Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, likitambua roho, siri za mioyo." Jinsi lilivyokuwa hasa wakati lilipofanyika mwili hapa duniani, katika Mwana wa Mungu, sasa linafunuliwa na Mwana wa Mungu kwani amekuja kumwita Bibi-arusi kutoka kwenye madhehebu hayo. "Tokeni kwake. Mkatengwe, asema Mungu. Msiguse vitu vyao vichafu, naye Mungu atawapokea."

273 Je! uko tayari kusalimisha uhai wako wote kwa Mungu? Kama uko tayari, simama kwa miguu yako, useme, "Nitalikubali, kwa neema ya Mungu, sasa hivi, kwa kila kitu kilichoko ndani yangu."

274 Haleluya! Mungu asifiwe! Mnamwamini Yeye? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Basi inueni tu mikono yenu na mwombe pamoja nami.

275 Tubuni makosa yenu. Utungu wa kuzaa! Ni vigumu kufa, lakini kufa sasa hivi. Kufa, toka kwenye imani yako ya kutokuamini. Toka huko. Hili ni Neno la Mungu lililodhihirishwa, kama tu lilivyokuwa wakati Yesu alipokuja duniani. Ni Yesu Kristo tena miongoni mwenu, akithibitishwa.

276 Ibrahimu alimpokea mwana mara moja, yule mwana aliyeahidiwa, baada ya jambo hilo kutukia.

277 Na Yesu anakuja tena. Huyo ni Roho Wake. Yeye amekaribia sana duniani, amekaribia sana kuja, hata Yeye yuko tayari kukupokea, kama wewe uko tayari kumpokea.

Sasa inueni mikono yenu na mwombe pamoja nami.

278 Bwana Mungu, jalia makuhani wote washikilie kwenye madhabahu. Jalia watu walie. Jalia Nguzo ya Moto na Nguzo

ya Wingu itende kazi ndani ya watu leo na kuwatuliza, Bwana, wapate kutambua Uwepo wa Mungu aishiye na mwenye nguvu. Tujalie, Bwana. Wapokee. Ninaomba sala hii kwa kila mmoja wao, katika Jina la Yesu Kristo.

279 Mjaze kila mmoja na Roho Mtakatifu, ambaye hana Roho Mtakatifu. Bwana, jalia ufufuo wa kampeni hii, mkutano huu, uanze sasa hivi uwe ni kumwagwa kukuu, kwenye nguvu, kwa Roho Mtakatifu. Jalia wagonjwa waponywe, vipofu waone, viwete watembee. Jalia dhihirisho la Mungu aliye hai liletwe kwenye uwepo wa watu, kama ilivyokuwa alasiri ya leo, na jalia watu walipokee. Katika Jina la Yesu Kristo, naomba.

280 Inueni mikono yenu sasa na msifu, na mpokee mlichoomba.

UTUNGU WA KUZAA SWA65-0124
(Birth Pains)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 24 Januari, 1965, katika Ramada Inn kule Phoenix, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2007 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org